# *YEHOVA-YIRE* [1]

Ketini. Hii ni nafasi muhimu sana, kurudi tena usiku wa leo. Na ni Baraka kubwa kwangu, kuja na kuzungumza nanyi kumhusu Bwana wetu Yesu, ambaye nina hakika kwamba wengi wenu mnamjua, ama ninatumaini mnamjua, katika kusamehewa dhambi zenu na—na kwa njia ya neema Yake, kwenu. Na pia naomba awakirimie, usiku wa leo, neema Yake zaidi. Tutakapoondoka hapa, na tuweze kusema, kama wale wanaotoka Emau, "Mioyo yetu iliwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani."

2 Sasa, kila asubuhi, ninaamini wana m—m—m—mtu wa uhusiano wa jamii kama yeye. Bw. Vayle hapa anafundisha so—somo, kwa namna fulani akijibu maswali na kuzungumza juu ya Maandiko. Je! hilo linafanyika hapa katika jengo hili? Papa hapa katika jengo hili, asubuhi. Na kama mtu yeyote yuko huru, na baadhi ya wahudumu, ama wengineo, wangetaka kutembelea, mbona, mtu yeyote anakaribishwa. Na Ndugu Vayle ni mwalimu mwenye kina kwa hakika. Hakika, yeye ana elimu nzuri.

3 Na kwa hiyo, nilisema hivi majuzi, la—laiti ningalikuwa na elimu. Inanibidi kutumia mifano, kufananisha kitu na kingine, kuelezea, mnajua. Sina elimu ya kutosha kulifafanua. Bali kwa namna fulani, ama kwa njia nyingine, Bwana hunisaidia kulieleza.

4 Na kwa hiyo ninakumbuka, wakati mmoja kulikuwa na m—mtu mmoja katika Maandiko, jina lake lilikuwa ni Yohana, na baba yake alikuwa ni kuhani. Kwa kawaida, wao waliambatana na shughuli za baba yao. Lakini kwa kweli yeye alikuwa na ujumbe; alikuwa amtangaze Masihi. Na sasa kama angalishuka akaenda kwenye shule ambayo baba yake alienda, wao walisema, "Sasa, unajua mpendwa Ndugu *Nanii*? Huyo kweli ndiye Masihi," karibu walimshawishi. Kwa hiyo, unaona, yeye hakuenda kwenye shule yoyote ya namna hiyo.

5 Alienda nyikani, ambako alijifunza mambo ya Mungu. Unaona jumbe zake, zilivyotoka? Yeye kamwe hakupata elimu yoyote. Alienda kule akiwa na umri wa miaka tisa, akatoka akiwa na umri wa miaka thelathini, akahubiri kwa miezi sita, kisha akauawa. Sasa tunaona ya kwamba yeye alitumia. . . Kasema, kama vile Mafarisayo walivyotoka, na Masadukayo, naye akasema, "Salala, enyi uzao wa nyoka!" Hao ndio aliokuwa amewaona nyikani; nyoka, kitu ambacho ni kichafu na kinachoteleza, na kidanganyifu. Unaona?

6 Sasa huenda mtu fulani angelisema, "Mbona, maskini wewe kijipande kidogo cha usumbufu kisicho na maana," ama kitu kingine. Lakini yeye . . .

7 Lakini, unaona, hakujua maneno ya kutumia, kwa hiyo yeye alisema tu, “Enyi uzao wa nyoka,” hao ndio aliokuwa amewaona nyikani. Kasema, “Ni nani aliyewaonya kuitoroka ghadhabu ijayo? Msianze kusema, ya kwamba ‘Tuna, sisi ni washiriki wa *hili* na ni washiriki wa *lile*,’ maana Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya,” yale aliyokuwa ameona, “kumwinulia Ibrahimu watoto. Na shoka limewekwa kwenye shina la mti.” Yeye alijua la kuufanyia mti mbaya. “Yeyote asiyezaa tunda zuri, hukatwa na kutupwa motoni,” kuuchoma mti mbaya.

8 Unaona, ujumbe wake wote ulihusu kitu fulani cha maumbile, alichofananisha nao. Watu wa kawaida wanauelewa huo. Na halafu wao . . . Nafikiri mara nyingine huenda ikawa ni bora zaidi kufanya hivyo kuliko maneno haya yote makubwa mno ambayo watu hujifunza shuleni.

9 Sasa, tulichelewa kidogo jana usiku, kwa hiyo tunajaribu kuwaruhusu mfumukane kwa wakati unaofaa tu, usiku wa leo, kama kweli tunaweza. Nami natumaini ya kwamba Bwana hataruhusu inyeshe sana kwa wingi usiku wa leo, juu ya paa hili la mabati, kwa hiyo tutaamini tu na—na kujaribu kumtumikia, kadiri tujuavyo.

10 Sasa hebu na tusimame tunaposoma Neno la Mungu, tunaposoma sasa kutoka katika Kitabu cha Mwanzo. Na tunaanzia kwenye mlango wa 22 na kifungu cha 7, tukisoma hadi cha 14, vyote pamoja.

> *Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akinena, Babaangu! naye akasema, Mimi hapa, mwanangu. Akasema, Tazama! moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa?*
>
> *Ibrahimu akasema, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu. Basi wakaendelea wote wawili pamoja.*
>
> *Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu, Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari kuni, kisha akamfunga . . . mwanawe mwenyewe, akamweka juu ya madhabahu, juu ya zile kuni.*
>
> *Ibrahimu akanyosha mkono wake, akakitwaa kisu ili amchinje mwanawe.*
>
> *Ndipo malaika wa Bwana akamwita kutoka mbinguni, akasema, Ibrahimu! Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa.*
>
> *Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala* usiweke . . . juu *yake; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo* umenizuilia . . . *hukunizuilia* nanii *wako . . . mwanao wa pekee.*
>
> *Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa*

*pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa ba. . . dala ya mwanawe.*

*Ibrahimu akapaita mahali hapo Yohova-yire, kama watu wasemavyo hata leo, Katika mlima wa* B*WANA* *itapatikana.*

11 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja tu tuombe.

12 Baba yetu wa Mbinguni, tunaambiwa na Neno hili, ambalo ni Mungu, ya kwamba, "Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno la Mungu." Na sasa, Baba, tunaomba ya kwamba utatukirimia mazingira ya somo hili, tupate kujifunza kama tunavyoambiwa na Biblia, ya kwamba, "Mambo hayo yote huko nyuma katika Agano la Kale yalikuwa ni mifano tunayopaswa kuona." Kwa wale wanaotii wito wa Mungu, wamebarikiwa. Wale wanaoukataa, wamelaaniwa. Kwa hiyo tunaomba, Baba, ya kwamba tutapata ufahamu, usiku wa leo, kwa ufunuo. Jalia Roho Mtakatifu atufunulie mambo yanayotuhusu sisi katika siku hii, yote yamefichwa katika siri hii kuu ya Mungu ambayo imekuwako tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

13 Ninataka kuzungumza juu ya somo, Bwana akipenda, kutoka katika wazo la: *Yehova-Yire*. Neno hili linamaanisha "Mungu atajipatia sadaka."

14 Nasi tunazungumza juu ya Ibrahimu, na huu ulikuwa ni katika wakati alipokuwa akimtarajia mwana wa ahadi. Ili kupata ukweli halisi wa jambo hili, tutarudi nyuma. Na hili lilikuwa ni katika mlango wa 22. Tunataka kurejea huko nyuma; nina Maandiko machache yaliyoandikwa hapa, ambayo ningetaka kuyarejea, ikiwezekana. Nami ninataka kuzungumza juu yake, na ninataka kuanzia kutoka mlango wa 12. Tutarudi nyuma tukaone mtu huyu Ibrahimu ni nani, na sasa ili—ilikuwaje kwamba Mungu alimchagua.

15 Tunajua ya kwamba ahadi ilitolewa kwa Ibrahimu na Uzao wake baada yake, na ni tukiwa ndani ya Ibrahimu tu ndipo tunakuwa warithi pamoja naye wa hiyo ahadi. Sasa Ibrahimu alikuwa na uzao, na uzao huo, kweli, ulikuwa, alikuwa na wazao wengi, wazao, bali alikuwa na Uzao mmoja ambaye alipewa hiyo ahadi. Alikuwa na Ishmaeli; na halafu baada ya Sara kufa, alioa mwanamke mwingine na akapata wana saba mbali na mabinti; nao wote ni uzao wa Ibrahimu, bali wa. . . wazao wa Ibrahimu, bali huo Uzao ndio uliokuwa na ahadi. Na huo Uzao, hasa, ni *imani* ya Ibrahimu, aliyokuwa nayo katika Neno la Mungu lililoahidiwa.

16 Sasa Ibrahimu, tunaona, sisi. . . hatokei mpaka tunapomwona hapa kwenye mlango wa 12. Mlango wa 11 wa Mwanzo, tunaona ya kwamba baba yake alishuka akaja

kutoka Babeli. Naye Ibrahimu alikuwa ni mtu wa kawaida tu, kama tu vile wewe au mimi, ama mtu mwingine yeyote. Naye alikuwa anakuwa, hasa, kile tungewazia, mzee. Alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano. Alikuwa ameoa dada yake wa kambo. Jina lake lilikuwa ni Sara. Na jina lake wakati huo, hasa, halikuwa Ibrahimu, lilikuwa ni Abramu. Na—na lake lilikuwa ni Sarai. Kwa hiyo tunaona ya kwamba alikuwa mdogo kwake kwa miaka kumi, ambalo lilimfanya yeye mwenye umri wa miaka sitini na mitano, naye miaka sabini na mitano.

17 Wao labda, alikuwa mkulima, waliishi kwenye bonde la Shinari kule, na waliishi maisha ya kawaida. Labda a—alitoka akaenda zake mchana, na kupata nyama yake kutoka kichakani, na kuchuma maforosadi, na kuishi maisha ya namna hiyo. Mtu wa kawaida tu, hapakuwa na jambo maalum kumhusu yeye. Lakini siku moja, Mungu alimwita. Hilo ndilo lililoleta tofauti, hapo Mungu alipotoa huo wito.

18 Na hivyo ndivyo ilivyo kwa maisha yoyote. Inamhitaji Mungu. Si yale wewe unayofanya; ni yale Mungu afanyayo. Unaona? Unasema, "Nilimtafuta Mungu. Nilimtafuta Mungu." Umekosea. Hakuna mtu anayemtafuta Mungu. Mungu humtafuta mwanadamu. Unaona? Si wewe unayemtafuta Mungu; Mungu ndiye anayekutafuta wewe.

19 Yesu alisema, "Ninyi hamjanichagua Mimi, bali Mimi niliwachagua ninyi." Unaona? Kwa hiyo umechaguliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, la sivyo hukuchaguliwa kabisa. Yeye alikuja tu kulikomboa jina hilo. Na wote wale ambao majina yao hayamo kwenye Kitabu hicho cha Uzima cha Mwana-Kondoo. . .kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ndio peke yao tu watakaokuwa kule, kwa vyovyote. Unaona? Ulichaguliwa katika Yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Wakati Mwana-Kondoo alipochaguliwa, ndipo ulichaguliwa pamoja Naye, kabla ya kuwekwa misingi.

20 Nawe, kama nilivyosema jana usiku, ni sifa ya mawazo ya Mungu. Unaona, hivyo ndivyo tu unavyoweza kuwa wa Milele, na aina pekee ya Uzima wa Milele. Kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na hiyo ni Mungu. Kwa hiyo, ni hayo tu, Yeye Ndiye aliye wa Milele.

21 Sasa tunaona ya kwamba Ibrahimu alipapata mahali hapo. Na Mungu, katika Agano la Kale, alionyesha mifano na vivuli, apate kuonyesha yale atakayofanya.

22 Sasa tunaona hapa ya kwamba Mungu alisena naye. Na jambo kuu, baada ya Mungu kumwita. . .Wito ambao Mungu alitoa ulikuwa ni wito wa kimbinguni. Lakini, hata hivyo, haukumfanya Ibrahimu asite, wakati wowote. Daima alijua ya kwamba mambo hayo yalikuwa ni Mungu. Hilo ni jambo kuu. Wakati. . .

23 Miito ya Mungu ni ya kimbinguni; hakuna kitu cha maumbile ya kawaida. Mungu huchukua ya kimbinguni na kuyafanya yatende kazi katika maumbile ya kawaida, bali miito ya Mungu ni ya kimbinguni. Biblia ilisema, "Karama na miito havina majuto." Unaona, vimekusudiwa awali na—na Mungu.

24 Sasa tunaona ya kwamba, katika jambo hili, ya kwamba Ibrahimu akiitwa, yeye alisikia sauti ya Mungu, Naye akamwambia jambo ambalo lilikuwa karibu haliwezekani kabisa. Yeye akiwa na umri wa miaka sabini na mitano, mke wake umri wa miaka sitini na mitano, hilo lingemfanya kuwa amekoma hedhi kwa karibu miaka ishirini, naye aliishi naye tangu alipokuwa msichana. Hawakuwa na watoto. Na, hata hivyo, alimwambia watapata mtoto, na kwa mtoto huyu ulimwengu wote, mataifa yote, yangebarikiwa. Sasa hilo ni jambo lisilo la kawaida.

25 "Naye Ibrahimu," Biblia ilisema katika Warumi mlango wa 4, "hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu, akimtukuza Mungu."

26 Ninaweza kuwazia, baada ya mwezi wa kwanza . . . Bila shaka, Sara, kama nilivyosema, alikuwa amekoma hedhi. Mwezi wa kwanza, ninaweza kuwazia Ibrahimu alisema, "Sara, unajisikiaje, mpenzi?"

"Hakuna tofauti."

27 "Vema, Mungu atukuzwe tutampata mtoto huyo, kwa vyovyote vile. Tutampata tu. Mungu alisema tutampata."

28 Sara, akashona vijiatu vidogo, na akanunua nguo za madoadoa na vipini, na kila kitu; akajiandaa, akijiandaa kwa ajili yake, maana alijua atampata. Mungu alisema hivyo. Unaona?

29 Mwaka wa kwanza ukapita. "Je! unahisi tofauti yoyote, mpenzi?"

"Hakuna tofauti hata."

30 "Mungu asifiwe! Utakuwa ni mwujiza mkuu sasa kuliko ilivyokuwa mara ya kwanza. Unaona, ni mwaka mmoja baadaye. Tutampata, kwa vyovyote vile." Kwa nini? Mungu alisema hivyo. Hilo latosha. Mungu alisema hivyo. Sisi . . . Mungu alisema hivyo.

31 Miaka kumi ikapita. "Unajisikiaje sasa, mpenzi?" Huyu hapa sabini na mitano, na yeye ana themanini na mitano.

32 Sasa ungeweza kuwazia mwanamume mzee na mwanamke kama huyo, leo, wakishuka kwenda hospitalini, na kusema, "Daktari, tunataka kufanya maandalizi. Tutaninii . . . "?

33 Mungu anakutaka uamini mambo mengine ya kuchekesha sana, bali Yeye daima huyafanya kuwa ya kweli. Mungu . . . Mtu anayemwamini Mungu, anafanya mambo kiwazimu kabisa, kwa ulimwengu.

34 Ungeweza kuwazia Musa, aliyefunzwa katika ninii yote—hekima yote ya Wamisri, kiongozi wa jeshi, ma—ma—ma—majeshi ya Misri. Na, hata hivyo, ilimchukua miaka arobaini kufunzwa kuhitimu hayo, kisha ikamchukua Mungu miaka arobaini kuondoa hiyo elimu kwake, muda tu uliochukua ulimwengu kuiweka ndani yake. Miaka arobaini zaidi, alimfundisha kupindukia, akatoa elimu yote, theolojia ndani yake. Naye alikutana naye mbali sana jangwani, ndipo akajua mengi zaidi juu ya Mungu, kwa dakika tano Mbele za Mungu, kuliko aliyojifunza katika miaka arobaini kutoka katika vitabu. Hiyo ni kweli.

35 Mungu hajulikani kwa elimu. Yeye anajulikana kwa imani. Na Mungu alizungumza naye kwa mambo ya kimbinguni. Na ni jambo la fedheha jinsi gani, wakati mwingine, Mungu anatufanya tutende.

36 Ungeweza kuwazia mzee, mwenye umri wa miaka themanini, akikimbia, nabii akimkimbia Mungu? Na katika Uwepo wa Mungu dakika tano: kesho yake asubuhi, (Ungeweza kumwazia?), mzee, masharubu yakining'inia chini sana namna *hii*; kipara chake kiking'ara; fimbo iliyopinda mkononi mwake; mke wake ameketi kwa kutanua miguu juu ya nyumbu, huku amemshika mtoto pajani mwake; akishuka kwenda zake!

"Unakwenda wapi, Musa?"

"Ninashuka kwenda Misri, kuiteka."

37 Unaona, "kuiteka," uvamizi wa mtu mmoja. Hilo linasikika lisilo la busara. Lakini, jambo lenyewe lilikuwa kwamba, alifanya jambo hilo, kwa kuwa Mungu alisema hivyo. Hilo latosha.

38 Mungu anaposema ni hivyo, ni mkataa. Ni—ni hilo tu. Kama Mungu alitoa ahadi, ambatanisha nafsi yako na jambo hilo. Kama unaweza kuamini jambo hilo, ambatanisha ninii yako. . . Kama huliamini, kaa mbali nalo; litakudhuru. Lakini kama unaliamini, dumu nalo, litakupeleka kwenye ushindi, kweli kabisa.

39 Sasa tunaona, ya kwamba, "Ibrahimu hakusita kwenye ahadi ya Mungu." Na wakati alipokuwa na umri wa miaka mia moja, naye alikuwa na tisini, ninaweza kumsikia; anazungumza kwa shida sasa, anazeeka sana na kuwa mnyonge, "Vema, Sara, mpenzi, unajisikiaje?"

"Abee, mpenzi, sijisikii tofauti."

40 "Haleluya! Tuta—tutampata, kwa vyovyote vile. Mungu alisema hivyo, hakuna la ziada. Mungu aliahidi." Alisema "alijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi."

41 Na sasa tunajiita Uzao wa Ibrahimu, Uzao wake wa Kifalme (si uzao wa Isaka), Uzao Wake wa Kifalme, Kristo; na tunasita katika ahadi yoyote, tunazozana nayo na kusema sivyo ilivyo, na

kuitilia shaka mawazoni mwetu? Ninatilia shaka kwamba sisi ni Uzao wa Ibrahimu tunapokuwa na wazo la namna hiyo ndani yetu. Uzao wa Ibrahimu hausiti katika chochote. Unaita vitu ambavyo havikuwa, kana kwamba vilikuwa, kwa kuwa Mungu alisema hivyo. Yeye ni Muumba. Anaweza kulitimiza. Aliahidi jambo hilo, na hilo latosha. Ni mkataa. Mungu anaposema jambo, hilo latosha kabisa. Sasa, kumbukeni, yeye alitaka jambo hilo . . . Kusingekuwa . . . Alimwambia . . .

42 Jambo lingine alilomwambia afanye, kujitenga sasa na jamaa yake na watu wake wote.

43 Mungu, ili kumfanya mwanamume ama mwanamke, mvulana ama msichana, kumtii, inakubidi kujitenga na kutokuamini kote, hiyo ni kweli, mpaka utakapojitenga kabisa na chochote kinyume na Neno hilo, na uliamini. Wewe . . . Mungu huagiza utengano mkamilifu.

44 Ni tofauti ya jinsi gani iliyopo leo katika shule zetu zinazowatuma wahudumu. Wanawashindilia tu na namna zote za kutokuamini na nadharia ambazo si za Kimaandiko kuliko namna fulani za kanuni za imani wanazobuni, na ndipo wanawatuma nje wakiwa na msingi kama huo. Si ajabu tumeangua kundi la akina Oswald na akina Jack Ruby, na kadhalika, kote nchini. Ukomunisti unaimeza nchi, kwa maana tuna wahubiri wa seminari na wahubiri wa kuatamiwa badala ya wana waliotumwa na Mungu, waliozaliwa mara ya pili, wakajazwa na Roho Mtakatifu, wana wa Mungu waliozaliwa kwa Moto, watoto wa Ibrahimu wanaoliamini Neno la Mungu kuwa ni la Kweli kabisa wala si kitu kingine ila ni Kweli tupu, washupavu, na wanaweza kusimama pale juu ya ahadi, mbele ya kitu chochote, na kukikabili, kwamba ni Kweli. Ni Neno la Mungu. Vema.

45 Sasa Yeye alisema, "Jitenge na jamaa yako yote, na watu wako wote, kila kitu, na ukanifuate Mimi."

46 Mungu hajabadilisha njia Yake. Mungu ni Mungu asiyebadilika. Jinsi Mungu anavyofanya jambo lolote, wakati mmoja, lazima alifanye jinsi iyo hiyo mara ya pili. Kumbukeni, wakati unapoweza kuona tendo la Mungu katika wakati wowote, kama Yeye . . . Kama—kama mtu alikuwa amepotea, Naye alimwokoa mtu juu ya msingi wa uamuzi wowote ule alioufanya, Yeye hana budi daima kudumu milele na uamuzi uo huo. Hawezi kuubadilisha. Mnaona? Yeye hana kikomo.

47 Sisi tuna kikomo. Ninaweza kujua zaidi kesho kuliko ninavyojua leo. Vivyo hivyo na wewe unaweza kujua zaidi mwaka ujao kuliko unavyojua mwaka huu. Unajua zaidi mwaka huu kuliko ulivyojua mwaka uliopita, bali si Mungu.

48 Yeye ni mkamilifu, hana mwisho. Kila kitu Yeye afanyacho ni kikamilifu. Hawezi kufanya uamuzi leo na kufanya ulio bora zaidi kesho. Uamuzi Wake wa kwanza ni mkamilifu.

Kwa hiyo, unaweza kuambatanisha nafsi yako kwenye chochote anachosema, ni Kweli.

49 Mungu aliitwa wakati mmoja kufanya uamuzi, jinsi ya kumwokoa mwanadamu, na jinsi alivyomwokoa ilikuwa ni juu ya msingi wa Damu iliyomwagika ya Asiye na hatia, katika bustani ya Edeni. Na mwanadamu amejaribu kila kitu ulimwenguni kumwokoa mtu, vinginevyo; wamejenga majiji, wamejenga minara, wamekuwa na mashirika, elimu, na chochote kile, na kitu hicho chote kimeshindwa kabisa. Kuna njia moja tu ambayo Mungu humwokoa mwanadamu, hiyo ni kupitia Damu iliyomwagika ya yule Asiye na Hatia. Hiyo ndiyo njia pekee. Huo ndio uliokuwa uamuzi wa kwanza wa Mungu. Yeye daima anadumu nao.

50 Kama Mungu alipata kumponya mtu kwa msingi aliomponyea, Yeye hana budi kumponya mtu mwingine wakati atakapofikia mahali hapo. Kama hakumponya, alifanya kosa wakati alipotenda mara ya kwanza wakati uamuzi huo ulipokuwa utolewe.

51 Kama akipata kufanya uamuzi kamwe, Yeye hana budi daima kudumu nao. Kama sivyo, alifanya uamuzi mbaya basi. Unaona? Na ni nani anayeweza kusema Mungu alifanya uamuzi mbaya? Unaona? Tusingeweza kusema jambo hilo. Kwa hiyo Mungu hana budi kudumu na uamuzi Wake daima. Kwa hiyo, wakati anapoufanya, huo ndio.

52 Kwa hiyo Yeye alisema, "Jitenge na jamaa yako yote, kila kitu, kutokuamini kote kunakoshuka kutoka Babeli huko juu."

53 Shirika kubwa la kwanza ulimwenguni lilikuwa ni Babeli, wakati lilipoiunganisha miji yote ipate kulipa kodi kwa mji huu mmoja, mfano halisi kabisa, itikadi hizi zote na mambo mapya yanayoonekana leo. Kama uliwahi kusoma kitabu cha *Babeli Mbili* kilichoandikwa na Hislop, na kadhalika, na urudi katika Mwanzo, utapata kujua Mwanzo ni chimbuko, mbegu, utaona itikadi hizi zote na kadhalika, zimewekwa vizuri moja kwa moja mle ndani.

54 Unaona, wale Mafarisayo wakaidi walioshuka wakaja kutoka kule, kutoka kwa mwanamke yule mwenye mizizi hiyo ya ajabuajabu na kadhalika, walishuka wakaja moja kwa moja katika siku za Yesu. Mafarisayo hawakuamini katika Roho wala chochote kile, nao walimkinza Yesu. Yesu alisema, "Waacheni. Kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, wote wawili huanguka shimoni. Waacheni . . ." Aliendelea kuhubiri moja kwa moja, na kuwaponya wagonjwa, na kufanya miujiza, na vivyo hivyo tu. Hilo halikumzuia, kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno. Neno linaendelea moja kwa moja, hata kutukie nini.

55 Kwa hiyo tunaona mambo hayo yanaendelea, na hatimaye yanafikia kuchanua hapa katika siku za mwisho. Kama vile

Yane na Yambre walivyoshindana na Musa, litakuwa ni jambo lilo hilo.

56 Sasa, utengano mkamilifu kutoka kwa kutokuamini kote. Na, kumbukeni, mzee wetu Ibrahimu kamwe hakubarikiwa kikamilifu mpaka alipotii vile hasa Mungu alivyosema afanye. Nasi kamwe, kamwe, kamwe hatutabarikiwa hata kidogo, na kupata baraka, mpaka tutakapotii yale Mungu aliyosema tuyafanye.

57 Jambo lingine ninalowataka mlione hapa katika mlango wa 12, ni kwamba kwa jumla agano hilo lilikuwa bila masharti kabisa. Halikuwa na masharti yoyote kwake. "Nimeninii tayari," si "kama wewe." Hakukuwa na kama kwake. "Tayari nimefanya jambo hilo." Alimpa Ibrahimu agano, bila masharti.

58 Na sasa ujue, katika agano la Adamu, ilikuwa, "Kama hutaugusa mti huu, basi nitafanya *hivi na vile*. Bali ukiugusa, basi itanibidi kufanya *hivi na vile*." Unaona, hilo lilikuwa limeambatanishwa na sheria.

59 Lakini katika agano hili, "Tayari nimekufanya baba wa mataifa mengi." Naye tayar-. . .Lote halina masharti. Agano hilo ni neema tupu, neema tupu kabisa. Jambo pekee walilopaswa kufanya kudumisha agano hili lilikuwa ni kukaa na kudumu humo nchini; na kila baraka, iliyoambatanishwa na agano hilo, ilikuwa pamoja nao. Jambo pekee walilopaswa kufanya lilikuwa ni kukaa katika nchi hiyo. Sasa tunaona, waliposhuka kwenda Misri, walipoteza baraka zao, bali si agano lao. Agano lilikuwa lingali lipo. Walipoteza baraka, bali si agano lao, kwa maana agano lao lilikuwa ni neema, bila masharti.

60 Na katika—katika Kutoka, mlango wa 19, Kuto-. . .Israeli walifanya moja ya makosa yao makubwa sana waliyowahi kufanya, ilikuwa ni wakati walipokataa neema na wakakubali sheria. Angalia kile neema ilikuwa imefanya. Ilibidi neema iwape mkombozi, ilibidi iwape nabii, pamoja na Nguzo ya Moto kumthibitisha kwa Neno lililohakikishwa, ilikuwa ni mwana-kondoo wa sadaka. Neema ilikuwa imewapa ufufuo mkuu. Neema ilikuwa imewafanikisha safarini, ikafungua Bahari ya Shamu, ikawavusha kwenye hiyo. Ikawakomboa kwa ishara na maajabu, yote kwa neema. Lakini wao walitaka kitu fulani ili wapate kujifanyia majina makubwa.

61 Sasa, kama hivyo sivyo watu walivyo siku hizi, ni jambo lile lile tu. Hawana budi kuwa hivyo, mwanadamu hana budi kujihusisha na jambo hilo mahali fulani. Na hapo ndipo Israeli walipofanya kosa lao kubwa sana, walipoikataa neema na kuchukua sheria, badala yake. Na ninii. . .Hata hivyo, lakini agano ambalo alifanya nao lingali lilikuwa bila masharti. Lingali ni jambo lile lile leo, tunaona hilo.

62 Ibrahimu, basi, baada ya kupewa masharti haya, alianza safari yake, akaendelea. Sasa tunaona yeye alitoka.

63 Na katika mlango wa 13, hatimaye alifikia mahali pa utiifu mkalimifu kwa Mungu. Sasa tunaona, katika mlango wa 13, ya kwamba Lutu. . . Kwanza, alimchukua baba yake, na mzee huyo siku zote alikuwa kwa namna fulani ni kikwazo. Naye alijaribu kulikokota kundi liambatane naye. Na wakati unapofanya hivyo, hapo ndipo unapoingia kwenye matatizo. Mungu alisema, "Jitenge."

64 "Vema, nitakwambia, hawaamini sawasawa kabisa, lakini. . . " Basi achana nalo. Hilo ndilo jambo pekee, kaa mbali kabisa nalo.

65 Basi ndipo huyu mzee, hatimaye, baada ya wao kumzika, basi, Lutu akawa pi—pingamizi kuu, kama tunavyosema. Tunaona ya kwamba alianza kunung'unika. Aidha wote wawili wakawa matajri, tena wote wawili wakawa na mambo mengi ya kushughulikia. Nasi tunaona basi ya kwamba Lutu alianza kugombana, wachungaji wake dhidi ya wachungaji wa Ibrahimu.

66 Na tunaona kwamba Yeye hakuninii, Mungu hakuwa ameona uaminifu mkamilifu katika. . . -ahimu, Ibrahimu, kutii yale aliyomwambia afanye, kujitenga kabisa na jamaa yake yote, kutoka kwa watu wake wote, na kumtumikia.

67 Kwa hiyo tunaona ya kwamba, Mungu akiwa anazungumza na Ibrahimu hapa, madhabahuni, na alikuwa amemwambia la kufanya. Hatimaye, Lutu, wakati swali lilipozuka kati ya Ibrahimu na Lutu; aliyekuwa mwana wa Harani ndugu yake, nao. . . Angekuwa ni mpwa wake. Na hatimaye akasema, "Hebu. . . Sisi ni ndugu sasa. Hatutakuwa na ugomvi wowote kati yetu. Sasa wewe, ukienda mashariki, nitaenda magharibi. Na kama ukienda magharibi, nitaenda mashariki. Sasa hebu na tutengane tu, na hatutaninii. . . Kuna maeneo makubwa kabisa hapa kwa ajili yetu sisi sote. Nawe nenda tu, wewe jichagulie tu." Sasa hiyo ilikuwa ni roho halisi ya Kikristo ndani ya Ibrahimu, kumpa hata adui nafasi ya kujichagulia. Na kwa hiyo alimwacha ajichagulie.

68 Naye Lutu, kama vile wengi sana walivyo siku hizi, aliona hiyo nafasi. Kama tu akiwahi kuondoka kwenye nidhamu hiyo kali, mbona, angeweza kujichumia dola chache, angeweza akawa mtu anayependwa sana na watu. Kwa hiyo akaelekeza macho yake chini upande wa Sodoma. Nayo ilikuwa ni nchi yenye maji mengi, na jiji kubwa, na kiwanda kizuri cha chumvi, na kadhalika. Wao, walikuwa na biashara ya kuuza bidhaa nchi za nje kutoka kule. Na—na halafu, tena, ulikuwa umejaa burudani, wanawake na rangi zao zote za Yezebeli na kila kitu, wakati wa burudani kwelikweli. Mke wake kwa namna fulani alijisikia kidogo namna hiyo, pia, kwa sababu, tunaona, baada ya yeye kuwa meya kule chini kwamba kwa na—namna fulani alipenda njia za hao watu. Na hilo ndilo jambo

pekee unalopaswa kufanya, ni kujichanganya na jambo fulani. Unaona?

69 Mungu anakutaka ujitenge, na—na uyaache kwa mbali sana mambo hayo mpaka huyaoni hata kidogo. Iwe kwamba, unataka kuona jambo moja, hilo ni Yeye na yale Yeye aliyoahidi.

70 Lakini mke wa Lutu, kwa namna fulani alipenda jambo hilo. Na, hapana shaka, kwa namna fulani alisema, "Mpenzi, sasa hivi ndio kwanza nitoke huko chini, na unaangalia jinsi hao wanawake wanavyovaa kule, na uangalie hao wasichana. Angalia jinsi wasichana wetu wanavyovalia. Kwa hiyo je! hudhani ya kwamba wao ni wa kisasa zaidi?" Loo, jamani! Kama hatujarudi moja kwa moja kwenye Sodoma nyingine, sijui ni kwa nini. Hapo tunaona.

71 Lakini Ibrahimu alidumu na ile ahadi. Ndipo tunaona, vile inavyoendelea, na ninii. . . walivyojitenga, na Lutu. Naye Ibrahimu alichukua nchi kame, njia nyembamba, akakaa juu ambako hakukuwa na malisho mengi kwa ng'ombe wake. Na, lakini, alikuwa tayari kuichukua njia hiyo, kwa kuwa Mungu alikuwa amemweka katika nchi hiyo, na humo ndimo alimotaka kukaa. Akiwa tayari kuitwaa!

72 Sasa wakati hatimaye, alipomtii Mungu kikamilifu, hatimaye wakati alipomtii Mungu kwa ukamilifu kabisa, kujitenga kabisa, hapo ndipo Bwana alipomtokea tena. Mpaka alipofanya jambo hilo, Bwana alikaa mbali na Ibrahimu. Lakini wakati alipotii kikamilifu, ndipo Lutu. . . Mungu akamtokea, akasema, "Ibrahimu, inua macho yako. Angalia mashariki, angalia magharibi, angalia kaskazini, angalia kusini, yote ni yako." Amina. Sasa, ninapenda hilo.

73 Na, unajua, jambo hilo ni kama vile ilivyokuwa wakati nilipookoka. Siku zote nilikuwa nimesikia kuhusu Mungu kuwa ni Mungu mkuu. Na, mnajua, nilipookoka, mimi. . . Mtu fulani alisema, "Sasa yote yakupasayo kufanya ni kujiunga na kanisa, na kuandikisha jina lako kwenye orodha hii ya kanisa hili hapa katika kanisa la Kibaptisti. Hayo tu ndiyo unayopaswa kufanya."

74 Lakini, unajua, siku moja niliona ya kwamba nilikuwa mrithi wa kitu fulani, ambacho ni—ni—nilitaka kuangalia humo na nione nilichokuwa nacho. Unajua, mimi niko hivyo tu. Kama nji—njia tao kubwa, ni mali yako, na—na kila kitu mle ni mali yako.

75 Hu—hujui unachomiliki mpaka utakapoanza kuangalia katika Biblia, kuona hizo ahadi. Amina. Watakuzuia usizipate wakiweza; bali ni zako. Kila ahadi ni kwa Ibrahimu na kwa Uzao wake baada yake. Amina. Kila ahadi ya Kiungu katika Neno ni mali ya Ibrahimu na Uzao wake, nawe ni mrithi wake. Mrithi! Loo, jamani! Ninapenda kuchunguza na kuona nina kitu gani. Kama mtu fulani akinipa kitu fulani, ninapenda

kukiangalia chote vizuri. Nami napenda kuichunguza Biblia nione kile kilicho mali yangu. Kila Uzao wa Ibrahimu unapaswa kufanya hivyo, unapozaliwa mara ya pili, ukajazwa na Roho wa Mungu, na Roho Mtakatifu akiwa juu yako, wewe ni mrithi wa kila mojawapo ya ahadi hizo.

76 Unajua, ni kama vile nilivyosema, njia tao kubwa, kwa kuwa tumebatizwa katika njia hiyo ya tao. Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika Mwili mmoja, na Mwili huo ni Kristo, ambaye ni Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, na warithi wa kila kitu kilicho ndani yake. Amina. Kila kitu kilichokuwa ndani ya Mungu, Mungu alikimimina ndani ya Kristo; kila kitu kilichokuwa ndani ya Kristo, Yeye alikimimina ndani ya mwaminio. Amina. Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, na Mungu ndani yetu! Kila kitu, kila ahadi katika kile Kitabu, ni yako kama unaweza kuamini, kama una imani ya kutosha kuikubali na kuiamini.

77 Unajua, ninaangalia kila mahali, kama nikipata kitu ambacho kidogo kiko juu mno, sijui kuna nini mle, nitachukua ngazi na kuisogeza karibu, na kuendelea kupanda mpaka nitakapokifikia. Hivyo ndivyo ilivyo, ahadi fulani katika Biblia, kama kitu chochote kinaonekana kana kwamba kwa namna fulani ni cha kisiri kwangu, ninaendelea tu kuomba mpaka nitakapokifikia. Hivyo tu. Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Endelea kuomba, endelea kushikilia, ukipanda juu, ukiamini, mpaka uninii . . . Wewe ni mrithi wake, una ahadi kwa kitu hicho, na una haki kwacho, na, "Ombeni nanyi mtapokea, kwa maana mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio."

78 Sasa tunaona ya kwamba Ibrahimu alitembea kote katika nchi hiyo. Mungu alimwambia, akasema, "Tembea kote nchini, iangalie vema. Kila kitu humu ndani ni chako. Kila sehemu yake yote ni yako. Yote ni mali yako."

79 Sasa tunaona basi, ya kwamba, katika mlango wa 14 wa Kutoka sasa ama . . . mlango wa 14 wa Mwanzo, samahani. Katika mlango wa 14 wa Mwanzo, Ibrahimu na Lutu walikuwa wametengana, naye Lutu hatimaye akaingia katika shida fulani. Na daima utaingia, wakati unapojitenga na waaminio, utaingia katika shida. Tunaona ya kwamba wafalme waliungana na wakafanya vita. Nao wakashuka wakaja wakauteka Sodoma, wakauteka Gomora, wakawateka wafalme wao wote wa mabondeni na mabonde, na kila kitu, na wakamteka Lutu. Na ni watu wachache tu waliokimbilia milimani.

80 Na walipofanya hivyo, mtu fulani aliyetoroka alikuja akamwambia Ibrahimu Mwebrania, akasema, ya kwamba, "Sodoma imeanguka, na Gomora, nao wamewachukua wafalme wao, na—na kadhalika, na kuwachukua watu wote, na vyakula vyao na kila kitu walichokuwa nacho. Kisha wakamchukua Lutu na mkewe, na binti zake, wanawake wote, nao wameenda nao."

81 Sasa, Ibrahimu, angalia roho hii ya Kikristo ikimfuatilia ndugu yake. Hata hiyo, ingawa, Lutu akiwa amekengeuka, amerudi nyuma, bado Ibrahimu alimpenda. Aliendelea tu kumfuatilia.

82 Ni kama tu vile Yesu, katika Wakati wa Kanisa la Laodikia. Hata hivyo, walimtoa kanisani mwao. Naye alikuwa nje, akibisha, akijaribu kurudi ndani. [Ndugu Branham anagonga mara saba juu ya mimbara—Mh.] Laiti angeliweza tu kumpata mtu fulani wa kufungua mlango ili aweze kuingia!

83 Hiyo hapo ile roho ya Ibrahimu, unaona, ikimfuatilia ndugu yake aliyeanguka, aliyevunjiwa heshima. Naye akamfuata, naye akawachukua watumishi wake mia tatu wa kiume na kuwapa silaha. Ndipo akamkuta huko Dani; huko ni mwisho kabisa wa Palestina pale. Naye akamkuta kule, na akajitenga usiku, na kuyafuatilia na kuyatwanga majeshi hayo kabisa, na kuwashinda hao wafalme, na kuwaua, na kurudisha yote yaliyokuwa yametekwa nyara.

84 Angalia, wakati aliporudi, ni picha nzuri jinsi gani hapa. Hiyo ndiyo sababu ninapenda tu kwa namna fulani kutangulia kulielezea hili kidogo, ili kwamba tupate ninii . . . kabla sijafikia kwenye somo langu la *Yehova-Yire*. Kama ukiangalia vile Ibrahimu alivyorudisha yote yaliyokuwa yamepotea, ndugu yake mkaidi na watoto, wakati alipokuwa akiwarudisha, wale wafalme walitoka wakaja kumlaki.

85 Ndipo Melkizedeki akatokea, "Ambaye alikuwa ni Mfalme wa Salemu, Mfalme wa amani, Mfalme wa haki, Mfalme wa Yerusalemu; bila baba, bila mama, bila mwanzo wa siku Zake, bila mwisho wa maisha Yake." Melkizedeki alikutana naye kwenye kuwau- . . . akija kutoka kumpiga mfalme, Ambaye mzee wetu Ibrahimu (Waebrania 7) alikutana na Mtu huyu na akatoa fungu la kumi, zaka. Hapana budi Mtu huyu alikuwa ni Mtu mkuu sana! Mnafikiri alikuwa ni nani? "Hakuwa na baba. Hakuwa na mama. Hakuwa na mwanzo wa siku Zake." Na yeyote Yule Aliye, Yeye angali yu hai. "Hakuwa na mwisho wa siku Zake. Mfalme wa Salemu, Mfalme wa amani!" Loo, Mtu huyu mkuu alikuwa ni Nani?

86 Na hebu angalia ni mfano wa jinsi gani tunaoupata hapa. Baada ya vita kwisha, baada ya mwaminio ha—halisi kumpiga adui, akavunja ngome na kujaribu kumteka ndugu yake, Uzao wa kweli wa Ibrahimu ukimrudisha ndugu mkaidi, Melkizedeki alijitokeza na kumpa divai na mkate, ushirika, kumpa ushirika baada ya vita kwisha, akampa ushirika baada ya vita.

87 Ni mfano mzuri sana wa wakati vita vitakapokwisha, hapa duniani, ushindi umepatikana. Yesu alisema, "Wataula upya katika Ufalme wa Baba," baada ya yule mkaidi kurudishwa. Ndipo jambo la kwanza tutakalofanya wakati tutakapoingia, baada ya vita kwisha, ni kuketi chini mezani katika Ufalme wa

Mungu. Na pale wale ambao wamepigana, na kuketi chini na kushinda, watavikwa haki ya Kristo, na halafu tena wanakula mkate na kunywa divai, katika Ufalme wa Baba katika ng'ambo ya pili. Ni picha halisi ya jinsi gani hii, ya Ibrahimu akitoka na kumpata Lutu na kumrudisha.

88 Sasa tunaona basi, ya kwamba katika mlango wa 15, tunaona jambo fulani zuri sana hapa. Kwa namna fulani na—napenda jambo hili, vizuri sana, kuona kwamba Ibrahimu alikuwa ni nani sasa, na Ibrahimu na Uzao wake baada yake. Tunaona hapa, ya kwamba baada ya Ibrahimu kufanya mambo haya yote makubwa; akimwamini Mungu, akishikilia ile ahadi, akijitenga, na daima akifuata njia ya—ya kutimiza amri za Bwana; tunaona ya kwamba Mungu alimtokea madhabahuni. Ndipo Ibrahimu akamwuliza swali, akasema, "Sasa, mrithi wangu ni nani ila—ila huyu Eliezeri wa Dameski? Na sasa Wewe uliniahidi Uzao. Nami ni—ninataka ufanye jambo fulani; ninataka unithibitishie ahadi hii."

89 Kadhalika Mungu alisema ya kwamba Yeye angeithibitisha kwa Ibrahimu, akithibitisha agano ambalo alikuwa amefanya kati Yake na Ibrahimu. Sasa Yeye atampa ishara ya kwamba itakuwa ni kweli. Hivi kwamba, hata ingawa yeye ni mzee, ana umri wa karibu miaka themanini na mitano sasa, lakini hata hivyo Yeye atamthibitishia, kwa ishara, ya kwamba atatimiza agano hilo.

90 Loo, nina furaha sana ya kwamba Mungu daima hutupa ishara, kwa sababu Yeye. . . Tunapaswa kujua, leo, ya kwamba saa hii tunayoishi sasa, kunapaswa kuwepo na ishara duniani wakati huu. Inatupasa kuitarajia ishara hiyo. Mungu kamwe hafanyi jambo lolote bila kwanza kuwapa watu ishara na onyo. Na ishara halisi hufuatwa na sauti, na sauti hiyo siku zote ni sauti ya Kimaandiko.

91 Sasa yeye atathibitisha agano hilo kwa Ibrahimu, ama Abramu, bado. Naye akasema, "Chukua ndama." Sasa, kumbukeni, huyo hapo ndama jike. "Na umchukue mbuzi jike wa miaka mitatu. Kila mmoja anapaswa kuwa wa miaka mitatu." Angalia, ndama wa miaka mitatu, jike; mbuzi wa miaka mitatu, jike. "Na kondoo mume," wa kiume. Kila mmoja mitatu, umri wa miaka mitatu, na hao hapo watatu. Watatu; jike, majike wawili, na mmoja wa kiume. Unaona? Umri wa miaka mitatu, sadaka safi; mwana-kondoo. . . ndama, mbuzi jike mwenye umri wa miaka mitatu, na halafu kondoo mume.

92 Kama ukitambua, kila kitu hapo kinaishia kwa ishara. Na sasa sipaswi kuhubiri fundisho kutoka hapa jukwaani, nami nina hakika hilo ni wazi sana hata mnaweza kuliona. Angalieni. Na akachukua wawili, ndege wawili. "Mmoja njiwa na mmoja hua," ambao ni wa jamii moja, njiwa na hua.

93 Sasa yeye alimkata yule mbuzi. . .yule kondoo vipande viwili. Akamkata yule kondoo mu—mume na mbuzi; na hao wengine. Akawagawanya, akawakata vipande viwili, akawalaza chini. Ila hua, yeye . . . na njiwa, hakuwapasua. Hiyo ilikuwa, bila shaka, mtu yeyote anayejua Maandiko, anajua huo ni uponyaji wa Kiungu. Unaona, uko kwenye maagano yote mawili. Na kwa hiyo tunaona, aliwaweka hapo. Uponyaji daima ni kwa imani katika Damu iliyomwagika, daima. Na lile agano la kale lilikuwa na uponyaji wa Kiungu, ni zaidi sana vipi Agano Jipya lilivyo nao? Mnaona? Kama agano la kale lilileta huo, vipi kuhusu lile Jipya, wakati, "Ni agano bora zaidi, linanena mambo bora zaidi, mambo ya juu zaidi, mambo makuu zaidi, mambo bora zaidi"? Agano Jipya!

94 Sasa tunaona katika jambo hili, ya kwamba Ibrahimu, wakati alipofanya jambo hili, basi angalia yaliyotukia. Sasa hili hapa jambo kubwa, muhimu sana. Sitaki ninyi m—m—mlikose hili. Kule kuthibitishwa kwa lile agano, kwa maneno mengine, ni ahadi, kwamba, "Mimi ni mwaminifu kwa yale ninayofanya ama yale ninayosema nitafanya," Mungu akimthibitishia Ibrahimu.

95 Na akachukua sadaka hizo na kuzichinja, na kuziweka ncha kwa ncha, pamoja, alipokuwa akizilaza chini; naye akawafukuza ndege toka kwenye sadaka hizo, kusudi ndege wasitue juu ya hiyo nyama mbichi, mpaka jua lilipoanza kutua, jioni. Na jua lilipotua, au lilipokuwa likitua, hapa alimwonyesha Ibrahimu yale atakayofanya katika siku za usoni, yale yatakayotukia.

96 Angalia, Yeye alimwambia Ibrahimu: Kitu cha kwanza alichoona kilikuwa ni hofu kuu ya giza likimwangukia. Kwanza, usingizi mzito sana ulimjia. Sasa, huo usingizi uliwakilisha mauti kwa binadamu wote. Kila mwanadamu hana budi kufa; mauti kwa wanadamu wote. Huo usingizi ulikuja juu yake; na kabla ya huo ilitokea hofu ha—ha—halisi ya giza; kisha tanuru ya moto ikatokea, na halafu Nuru ndogo inayowaka ilienda katikati ya agano hilo, ikaenda katikati ya sadaka hizo, ikazigawanya. Sasa hilo lina maana gani? Linamaanisha ya kwamba kila mwanadamu hana budi kufa; na kwa kweli, baada ya hilo, anastahili kwenda kuzimu; hiyo ni kweli, kwenye giza, giza la nje, ametengwa na Mungu; bali hiyo Nuru iliingia, na ikaenda katikati, ikizigawanya sadaka hizo. Kama unaelewa, sisi . . . Lile agano!

97 Kama vile sisi Wamarekani, je! tunafanyaje agano? Vema, jambo la kwanza tunalofanya, tunasema, tutafanya mapatano fulani ya biashara ama chochote kile, kwa kawaida tunatoka tunaenda kula; na tunaketi, tunazungumza kidogo, halafu tunatoa mapendekezo yetu; kisha tunapeana mikono. Tunasema, "Nipe mkono!" Hilo ndilo agano letu. Hiyo ndiyo ahadi yetu.

98 Sasa, huko Japani, je! mnajua jinsi wanavyofanya agano huko Japani? Wao pia wana kitu cha kula; kisha wanachukua

chupa ndogo ya chumvi, nao wanarushiana chumvi mmoja kwa mwingine. Hilo ndilo thibitisho la agano hilo.

99 Sisi tunapeana mikono, tunasema, "Limeidhinishwa, rafiki yangu. Ninaliamini. Nitadumu pamoja na wewe. Ni ahadi."

100 Kijapani, huko Japani, wanarushiana chumvi. "Limeidhinishwa, rafiki msiri. Huo ndio mwisho wake." Huo ndio mwisho wa ugomvi wote basi. Wao, walifanya agano, wakalithibitisha, kwa kurushiana chumvi wao kwa wao.

101 Lakini katika zamani za kale. Je! ninaweza kuchukua moja ya hizi? [Ndugu Branham anachukua kipande cha karatasi—Mh.] Zamani za kale, hivi ndivyo walivyofanya agano. Tulifanya mapatano, na tukachukua mapatano hayo na kuyaandika namna *hiyo*. Halafu tukamchinja mnyama, sadaka, tukampasua, tukamtandaza kama ilivyokuwa katika wakati wa Ibrahimu pale. Kisha tukasimama katikati ya agano hili, mimi na wewe, nasi tukaweka nadhiri kwa Mungu. "Kama tukishindwa kuweka agano hili, na tuwe kama sadaka ile iliyokufa mahali petu. Damu ya sadaka ile na iwajibike juu yetu. Na tufe kifo kile kile, kama tukishindwa kutimiza agano hili."

102 Ndipo lote linachorwa, ama linaandikwa kwenye kipande cha karatasi namna *hiyo*. Ndipo kinararuliwa vipande viwili, namna *hiyo*. [Ndugu Branham anararua kipande cha karatasi vipande viwili—Mh.] Sasa wewe unachukua nusu, nami ninachukua nusu. Na sasa, unaona, huwezi kufanya nakala ya hicho hata kidogo, hasa sana wakati limeandikwa kwenye ngozi ya kondoo. Unaona, usingeweza kufanya nakala yake hata kidogo. *Hiki* hakina budi kuumana na *hicho*, kulifanya liwe kweli. Na ndipo tunapokutana, ninabeba kipande kimoja, nawe unabeba kipande hicho kingine. Ndipo basi tunapokutana, na agano hili linapaswa kufanywa, na nadhiri zetu zinabidi kutimizwa, basi kipande changu cha karatasi hakina budi kuumana sawasawa na kipande chako cha karatasi, na kwa hiyo wewe ndiwe ambaye tuko pamoja katika agano hilo.

103 Kile Mungu alichokuwa akionyesha pale kwamba anakifanya, ni kwamba Mungu Mwenyewe alikuwa akishuka apate kufanyika mwili, Naye alikuwa anaenda kuwa katika agano hilo. Ndipo Mungu akamchukua Kristo, Roho; Mungu Yehova alimchukua Kristo, pale msalabani, na akampasua vipande viwili. Aliirarua nafsi Yake na akaiweka huko Juu, kisha akauchukua mwili akaulaza kaburini. Kisha akauinua huo mwili, katika ile asubuhi ya ufufuo; ndipo akamrudisha Roho aliyekuwa juu Yake, apate kuwa juu ya Kanisa. Hilo, hilo ni thibitisho lile lile katika siku hizi za mwisho, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele," ambapo agano lilo hilo litapaswa kuwa ndani ya watu.

104 Utalipataje kupitia elimu? Utalipataje kwa njia yoyote mbali na thibitisho la Yesu Kristo, aliye hai, ambaye amefufuka katika

wafu na ameketi katika Ukuu huko Juu, usiku wa leo? Huku Roho yule yule aliyekuwa juu Yake, yuko juu ya Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, katika siku za mwisho, akithibitisha na kuhakikisha ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Amina. Linakufanya ujisikie kubarikiwa, sivyo? Hilo hapo, katika agano halisi, "Nitaandika agano Langu mioyoni mwao." Yesu alisema, "Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya."

105 Tunapokuja hapa Sodoma, katika dakika chache, angalia jinsi ilivyo, jinsi linavyotukia pale, jinsi ambavyo ndivyo hasa ahadi hiyo ilivyo kwa ajili ya siku ya mwisho na yale Yeye angefanya.

106 Alikuwa akithibitisha jambo hilo, akionyesha ya kwamba Yeye. . .Yeye aliupasua mwili wa Yesu vipande viwili, akaichukua Roho, akauchukua mwili akauweka mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu; kisha akashusha sehemu hiyo nyingine, ile sehemu aliyoipasua, hiyo Roho juu yetu, ambayo inaitwa Roho Mtakatifu. Na Uzima ule ule uliokuwa ndani ya Kristo uko ndani yako, hiyo inaonyesha Yeye ni Mkombozi wako. Amekufanya mwana mwenye mamlaka kwa Mungu, na sasa sisi ni wana na binti za Mungu, tukiwa na Roho wa Kristo. Amina.

107 "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Kubwa kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu." Amina.

108 Roho aliyekuwa ndani Yake yuko juu yako, Uzima wa Milele. Ndiye mwenye kutoa Uzima wa Milele. Yeye ni Mkombozi, apate kuwarudisha wale walioanguka katika kule kuanguka, katika jamii ya binadamu, kuwarudisha kwa Mungu. Na Roho aliyekuwa ndani ya Kristo yumo ndani yako. Na kama roho ya—ya Dillon fulani ilikuwa ndani yangu, ningekuwa na bunduki. Kama roho ya msanii ilikuwa ndani yangu, ningechora picha. Kama Roho wa Kristo yuko ndani yako, kazi za Kristo utazifanya. Amina. Hiyo ni kweli. Uhai uliokuwa ndani Yake uko ndani yako.

109 Hamisha uhai kutoka kwenye kitu chochote uuingize kwenye kitu kingine. Kama ungeweza kuchukua uhai wa—wa boga na kuuweka katika mtikiti maji, ungezaa maboga, kabisa. Ukitoa uhai kutoka kwenye mpichi, na kuutia katika mpea, utazaa mapichi, kwa maana uhai ulio ndani ya mti huo hutoa thibitisho lake.

110 Na hivyo ndivyo ilivyo na Uzao wa Kifalme; kupitia kwa Isaka ulikuja uzao wa kawaida, ambao ulikataa Hilo. Pale msalabani, kutoka kwa Efraimu kwenda kwa Manase, ilihamishwa, ile baraka kutoka mkono wa kuume ikaingia mkono wa kushoto; ama mkono wa kushoto ulikuwa ni wa kushoto, kitinda mimba zikamwendea kifungua mimba; kupitia

hapo hali yote ilibadilishwa kutoka kwenye uzao wa kawaida wa Isaka, ambao ulimkataa Kristo, na kanisa la kawaida leo ambalo lingali linamkataa Yeye.

111 Bali Uzao wa Kifalme wa Mungu, wa kiroho, unaoamini, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu ambao unaamini kila Neno la Mungu, kuna thibitisho la Yesu Kristo aliye hai, aliyefufuka ndani yao. Amina. Amina. Loo, jamani! Unaona, lilikuwa ni jambo lile lile, kanisa lote halina budi liwe jamii moja.

112 Wakati lilipofananishwa katika uzao wa kawaida, angalia, Isaka na Rebeka walikuwa ni binamu wa karibu, wenye jamii moja ya damu, baba wale wale; unaona, baba zao walikuwa ni ndugu, iliwafanya kuwa binamu wa karibu, bibi-arusi na bwana arusi.

113 Na katika Adamu na Hawa, wote walikuwa ni Adamu, hapo kwanza. Mungu alitoa ubavu mmoja kutoka ubavuni mwake na kumfanya mwanamke, kisha akachukua roho ya kike kutoka kwa Adamu na kuiweka katika mwanamke.

114 Kwa hiyo wakati mwanamke anapotenda kama dume, kuna kitu fulani. . .kuna upotovu fulani hapo mahali fulani. Na wakati mwanamume anapotaka kuwa dondoadume mkubwa, kuna kasoro fulani mahali fulani. Mungu alimwumba mwanamume na kumvalisha kama mwanamume, na mwanamke kama mwanamke. Yeye daima anawadumisha wawe hivyo. Amina. Unapowaona wakifanya jambo tofauti, kuna kasoro fulani. Jambo hilo limepotoshwa. Na jambo lote limekuwa ni kundi la wapotovu. Hiyo ni kweli kabisa. Jamii yote, kizazi chote, ni, "kitu hicho chote ni kidonda chenye usaha," kama vile Biblia ilivyosema. Ni vigumu kupata uzima mahali popote. Unajua hiyo ni kweli. Ni vigumu kwako kupata wo—wote miongoni mwao huko nje. . .Lakini toka uende mtaani, ni vigumu kumpata mwanamume halisi; madondoadume kama niliowahi kuona. Na wanawake, wanavaa suruali ndefu, wanakata nywele zao, wanajipodoa midomoni, wanavuta sigara, wanajaribu kujifanya mwanaume. Unataka kuwa mwanamume kwa sababu gani? Unapaswa kuwa bibi.

115 Niliona tangazo, lililosema, "Meza za mabibi," kwenye baa.

116 Nikasema, "Kamwe hukupata mteja." Bibi hataenda mahali kama hapo. La, bwana. La, bibi hataenda. Mwanamke huenda akaenda, bali si bibi. Hataingia mahali kama hapo. Lakini haya basi, unaona.

117 Mungu alitenganisha, akakata. Unaona, ule Mwili, Bibi-arusi wa Kristo, hana budi kurudi moja kwa moja kwenye hali ya kwanza. Sasa Hawa alikuwa . . .

118 Hawa alikuwa ni nini? Yeye na Adamu walikuwa ni mmoja. Waliitwa Adamu. Walikuwa ni roho. Wakati alipomfanya mtu, kwa mara ya kwanza, Yeye alimfanya kwa mfano Wake Mwenyewe. Na Mungu ni Roho. "Katika mfano wa Mungu

alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba." Yeye alikuwa . . . na halafu bado hakukuwa na mtu wa kuilima ardhi. Ndipo Mungu akamwumba mtu kutoka katika mavumbi ya ardhi na akaweka roho huyu wa aina mbili ndani yake, na huyo alikuwa ni Adamu wa kwanza.

119 Ndipo wakati alipomtenganisha Hawa kutoka kwa Adamu, Hawa alianguka kwa kutokuliamini Neno. Hiyo ni kweli. Hapo ndipo kanisa liliposhindiwa leo, kutoliamini Neno!

120 Lakini katika kisa hiki, kwa huo Uzao wa Kifalme, walioitwa, wakakusudiwa tangu zamani Uzima wa Milele, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, wao wanaliamini hilo Neno. Sijali nini kinachokuja ama kinachoenda, wanacheka kiasi gani, ni nani anayesema jambo *hili*, *lile*, ama *linginelo*, wao wamekusudiwa Uzima wa Milele. Naye anarudi moja kwa moja alikotoka. Yeye pamoja na Mpenzi wake, Kristo, ni mmoja. Ule Uzima, Roho aliye ndani ya Kristo, yumo ndani ya Kanisa. Hilo ndilo agano lao la Milele, hapa. Unaona? Mungu alimchukua Roho wa Kristo, akampasua, kwenye ile sadaka pale Kalvari; kisha akaichukua hiyo Roho, akauinua huo mwili na kuuweka kwenye mkono wa kuume wa kile Kiti cha Enzi cha Mungu na Ukuu huko Juu. Hiyo ni kusema, kila kitu Mbinguni kinatawaliwa na Yeye. Halafu Roho yule aliyekuwa juu Yake, alirudi; Roho yule yule, si Roho mwingine, Roho yule yule alimjia Yeye, apate kuthibitisha lile agano kwa Uzao wa Kifalme.

121 Na katika siku za mwisho tunapaswa kuona jambo hilo, kulingana na Maandiko. Na kabla Bibi-arusi wa Kristo hajapata kutwaliwa juu, inabidi kuwe na huduma inayolingana na hiyo kabisa. Amina. Nina furaha sana kusema, usiku wa leo, ya kwamba ninajua hiyo ni Kweli. Amina. Ikilingana, ikithibitisha lile agano!

122 Yeye alilithibitisha pale, akamwonyesha yale atakayofanya, akilithibitisha lile agano. Msomi yeyote wa Biblia anajua ya kwamba hapo ndipo alipolithibitisha lile agano kwa Ibrahimu. Alikuwa akifanya nini? Akionyesha kwa mfano, kile ambacho atafanya, na sadaka hizi.

123 Na sasa tunachelewa, wala sitakuwa na wakati wa kuzitenganisha sadaka hizi. Itanibidi labda kufanya hivyo kesho usiku, lakini, angalieni, kuonyesha kwamba hizo, kile sadaka hizi zilichomaanisha. Lakini, mnaona, Yeye alilithibitisha, akionyesha ya kwamba katika siku za mwisho . . .

124 Sasa mtu yeyote aliyepata kusoma historia ya kale, anajua ya kwamba hivyo ndivyo walivyofanya agano. Waliliandika, kisha wakalirarua, na kupeana; mmoja akachukua kipande kimoja, na mwingine hicho kingine. Iliwabidi kurudi, juu ya sadaka, kutoa sadaka yao. Hivyo ndivyo Ibrahimu alivyomfanyia nanii . . . huko Gerari, na kadhalika, wakati alipoenda kule, ambako walitoa madhabahu . . . walitoa sadaka yao na kufanya mapatano yao,

na kuirarua namna hiyo. Naye Mungu alifanya jambo lile lile, akionyesha pale atakayofanya kwa I-. . .

125 Suala lilikuwa, "Uko wapi—uko wapi huu Uzao ulioniahidi? Wapi? Nitakuwaje hivyo? Watu wananicheka, wakisema, 'Ibrahimu, baba wa mataifa, imekuwa ni miaka kumi na mitano. Sasa wewe una umri wa miaka themanini na mitano, ama—ama tisini. Wapi, wapi, wapi, wapi watoto wako wote? Una watoto wangapi sasa, baba wa mataifa?'" Unaona, wakimdhihaki. Lakini yeye hakusita. Alishikilia moja kwa moja. Walidhihaki, wakasema, "Baba wa mataifa, sasa hebu tuone, una watoto wangapi wakati huu?" Unaona, wakitaka kumdhihaki, kwa maana alikuwa ameshikilia ahadi za Mungu, akiamini ya kwamba Yeye anaweza kutimiza yale aliyoahidi. Ye—yeye anaweza hata na zaidi. Yeye ana . . .

126 Anaweza kutoa sadaka Yake Mwenyewe. Yeye ni Yehova-Yire. Anaweza kutoa na kufanya njia kwa ajili ya yale aliyoahidi. Naye alithibitisha lile agano kwake kwa kumwonyesha jinsi atakavyolifanya, akimchukua Kristo na kuurarua Uhai kutoka Kwake, na kuushusha katika siku za mwisho juu ya . . .

127 Sasa tutamalizia hilo katika Maandiko, juma hili, kuwathibitishia jambo hilo, ya kwamba agano hili halina budi kuthibitishwa kwa Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, ambao ni watu kutoka kwa Mataifa, si Wayahudi, "watu kutoka kwa Mataifa, kwa ajili ya Jina Lake," wakilichukua kwa ajili ya Jina Lake. Kanisa ambalo lina Jina Lake litarudi ndani Yake, kwa maana ndivyo lilivyo, Uhai wake.

128 Sikilizeni, wakati katika Siku ya Pentekoste, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka katika Siku ya Pentekoste, Uhai huo ulipewa Kanisa. Na Kanisa hilo lililotoka moja kwa moja na kutoa, waliandika nyuma ya Kanisa hilo Kitabu cha Matendo, juu ya yale liliyofanya, kwa sababu ilikuwa ni Kristo ndani ya wale mitume.

129 Sasa Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 15, "Mimi Ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi." Sasa, Mzabibu hauzai tunda. Tawi ndilo linalozaa tunda. Linatiwa nguvu na Mzabibu. Vema, sasa, kama tawi hilo, la kwanza lililotoka kwenye mti huo, lilitoa Kitabu cha Matendo; kama hilo likiwahi kuzaa tawi jingine, utakuwa ni Uhai ule ule.

130 Miezi michache iliyopita, nilikuwa nimesimama pamoja na rafiki yangu wa thamani, John Sharrit, huko Phoenix. Mimi ninaishi Tucson, kama mjuavyo. Na kwa hiyo nilikuwa huko Phoenix, Ndugu John Sharrit, ndugu Mkristo mzuri sana. Naye alikuwa maskini sana, maskini hohehahe, na Bwana amembariki. Na—na wakati nilipokwenda Phoenix kwa mara ya kwanza, miaka kadhaa iliyopita, yeye hakuwa na watoto. Na—naye alitaka watoto. Na—nao, maskini, wakifanya kazi kwenye barabara, wakibomoa matofali ya zege, kama senti

ishirini na tano, thelathini kwa saa. Ndipo akashuka akaja kule, naye akaamini kila Neno la Ujumbe. Ndipo akasema, “Je! utaniombea?” Ana watoto watano sasa.

131 Na hilo, mbali na jambo hilo, yeye anatoa dola milioni tatu hadi nne kila mwaka kwa huduma ya Kristo. Na hiyo ni kweli. Nilikuwa pamoja naye hapa, si muda mrefu uliopita, tukiangalia shamba lake la pamba. Yeye alinunua wilaya nzima, alikuwa na Wameksiko elfu moja mia tano wakilishughulikia. Na alikuwa, miaka kumi na mitano iliyopita alikuwa akibomoa matofali ya zege, kwa senti ishirini na tano kwa saa.

132 Alinipeleka kwenye msitu wake mkubwa wa matunda chungwa. Nami nikaona mti wa kuchekesha mno, pale, niliopata kuona maishani mwangu. Ulikuwa ni namna fulani ya mti, ulikuwa na matunda ya kila aina juu yake. Nami nikaangalia, nao ulikuwa na machungwa, ulikuwa na malimau, ulikuwa na mabalungi, ulikuwa na machenza, ulikuwa na makangaja. Nafikiri kulikuwa na aina tisa mbalimbali za matunda, ama kumi. Ndipo nikasema, “Ule ni mti wa aina gani?”

133 “Loo,” akasema, “hilo ni jaribio dogo tu, Ndugu Branham.”

134 Nikasema, “Loo, kumbe.” Kisha nikasema, “Yote inaishi kwa ule mti mmoja?” Nikasema, “Ni mti wa aina gani, kwanza?”

135 Akasema, “Ni mchungwa. Huo ni mchungwa kitovu.”

136 Nami nikasema, “Ni kweli?” Nikasema, “Jamaa hawa wengine wanafanya nini pale?”

Naye akasema, “Wamepandikizwa humo.”

137 Nikasema, “Loo, kumbe.” Nikasema, “Naelewa.” Nikasema, “Sasa, sasa mwaka ujao, kila kitu kitarudia kuwa ni mchungwa, sivyo?”

138 Kasema, “Loo, la.” Kasema, “La, limau litazaa limau.” Akasema, “Ninii . . . na mbalungi utazaa balungi, na mchenza utazaa chenza.”

Nikasema, “Kutoka kwenye mchungwa?”

Akasema, “Ndiyo, bwana.”

Nikasema, “Sioni linawezaje kufanya hivyo.”

Kasema, “Yote ni matunda jamii ya chungwa.”

Nikasema, “Vema, Bwana asifiwe! ninaona jambo fulani.”

139 Angalia! Loo, ndugu, wakati Roho Mtakatifu huyo alipoingia kwenye Mzabibu huo, na ukazaa kutoka kwenye Mzabibu wake kwa tawi la kwanza, nao wakaandika Kitabu cha Matendo nyuma yao. Kama mti huo ukipata kuzaa tawi jingine asilia, utazaa kitu kile kile. Itakuwa ni Yesu Kristo. Sasa tuna Methodisti, Presbiteri, Baptisti, Lutheri, chochote kile kimepandikizwa ndani yake, kikizaa matunda ya kimadhehebu; bali kama huo ukiwahi kuzaa tawi jingine, litakuwa ni Neno

la Mungu la kweli, lililojaa Kristo na ambalo kiini chake ni Kristo.

140 Na, kumbukeni, kumbukeni ule ujumbe wa *Mti wa Bibi-arusi*. Wengi wenu huchukua kanda. Jinsi ambavyo mwenye shamba alikuja, nao ulikuwa ukizaa matunda mabaya, kwa hiyo akaukatilia mbali, akaukatilia mbali, akaendelea kuupogoa, kuupogoa. Lakini Yoeli alisema, "Yaliyosazwa na tunutu, yameliwa na madumadu; yaliyosazwa na tunu-. . . yaliyosazwa na madumadu, yameliwa na kitu kingine." Tunaona ya kwamba wadudu hao ni wadudu wale wale, ila tu ni katika hatua nyingine. Na yaliyosazwa na Mlutheri, yameliwa na Mmethodisti; yaliyosazwa na Mmethodisti, yameliwa na Mbaptisti; yaliyosazwa na Mbaptisti, yameliwa na Wapentekoste. Kitu hicho chote kimekatwa kabisa.

141 Bali Mungu alisema, "Nitarudisha, asema Bwana, miaka yote. Nitatuma Kanisa lingine, katika siku za mwisho. Nitarudisha hizo Nguvu za asili tena. Ni-. . .Wakati wa jioni, kutakuwako Nuru." Chini kabisa katika moyo wa mti huo, haidhuru ni matawi mangapi yanapogolewa, utatokea Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu! Haleluya! Mungu aliahidi jambo hilo. Mungu atalifanya. Alisema angelilifanya. "Nitarudisha miaka yote iliyoliwa na madhehebu. Nitarudisha miaka yote. Nimepogoa kitu hicho kabisa, bali hata hivyo Mzabibu utatokea toka kwenye moyo wake. Atakuwa kama mti uliopandwa karibu na mito ya maji, mtu ambaye anatafakari Neno la Mungu, mchana na usiku," si kanuni ya imani wala madhehebu, "bali anayetafakari Neno, mchana na usiku. Atakuwa kama mti uliopandwa karibu na mto wa maji; matawi hayatakauka. Atazaa matunda yake katika majira yake." Mungu aliahidi jambo hilo.

142 Mungu, akipasua, akitoa, akikata vipande viwili, akijitenganisha Mwenyewe, akijigawa Mwenyewe. Alifanya jambo lile lile kwenye Siku ya Pentekoste, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka. Ile Nguzo ya Moto ilishuka, iliyowafuata Israeli, sote tunajua hiyo ilikuwa ni Logos, hiyo ilikuwa ni Kristo. Na wakati iliposhuka, kwenye Siku ya Pentekoste, ilifanya nini? Ilijigawanya Yenyewe, na ndimi za Moto zikakaa juu ya kila mmoja wao. Mungu akijigawanya Mwenyewe miongoni mwa watu. Loo, ndugu, mnaweza kuwa kitu kimoja, mkiwa na Roho ile ile iliyokuwa ndani ya Kristo.

143 "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya. Kubwa kuliko hizi, ama *nyingi* zaidi kuliko hizi," fasiri iliyo sahihi "kwa kuwa ninaenda kwa Baba. Bado, kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena, hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi," kiwakilishi nafsi, "nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, wakati wa mwisho, utimilifu wa dahari." Yeye aliahidi kufanya jambo hilo. Enyi Uzao wa Ibrahimu, Yeye yupo hapa sasa. Ananinii . . .

144 Tupo hapa, siku chache zilizopita, tukisherehekea kufufuka Kwake, ambaye Mungu alimfufua. Tunashuhudia jambo hilo. Tunaliimba. Naye anaweza kutokea na kufanya jambo alilofanya, kama tu vile alivyofanya kabla ya kufufuka Kwake, tungeliita jambo hilo, "mpiga ramli, ibilisi, Beelzebuli," tulifungie nje ya kanisa. Tunafanya hivyo kwa nini? Hatuna budi kutimiza Maandiko, ya kwamba, katika Wakati wa Laodikia, Neno, ambalo lilikuwa ni Kristo, lilitolewa nje, [Ndugu Branham anagonga mara nne mimbarani—Mh.] akibisha mlango, akijaribu kupata ushirikiano kutoka mahali fulani, apate kuingia na kujitambulisha.

145 Lakini tawi litachipuka tokea Pale, kwa hakika kama chochote kile!

146 Nilimwambia Ndugu Sharrit, "Basi ni tawi la namna gani utakalochipusha mwaka ujao? Je! litakuwa ni mchungwa? Litakuwa ni la mlimau? Litakuwa . . . "

147 "Naam, litakuwa ni tawi la asili," alisema. "Utakapotoa tawi lake wenyewe, litakuwa ni la mchungwa, kama tu ulivyokuwa pale mwanzo."

148 Na wakati Uzao halisi, ulio hai wa Ibrahimu utakapochipuka, Roho yule yule aliyekuwa ndani ya Yesu Kristo ataishi miongoni mwao, kila Neno litaitikiwa kwa "amina." [Ndugu Branham anapiga mimbara mara nne—Mh.] Wanaliamini. Si, "*Hili* lina pumzi, na *Lile* halina pumzi." Wanaamini Jambo lote zima, maana ni Neno la Mungu.

149 Je! mnaamini jambo Hilo, usiku wa leo, kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ninaliamini.

150 Nimekwisha kuhubiri hapa sasa mpaka muda mrefu umepita. Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja. Nami nitamalizia hili kesho usiku. Niliahidi sitawacheleweshа.

151 Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na kuthibitishwa. Lilitatuliwa kwa Ibrahimu, wakati alipoliona kwa imani, akaenda moja kwa moja, bila kusita katika kutokuamini. Hakusita. Sasa vipi kuhusu Uzao Wake wa Kifalme, sisi ambao tunadai, sisi Wakristo wa siku hii, ambao tunadai kubusu kikombe kile kile ambacho Yeye alikinywea, tukiwa na Roho Wake yule yule ndani yetu, na kumwona Yeye akithibitisha ahadi Yake ya kuwa hapa pamoja nasi?

152 Ile ahadi, kuifanya itimilike, haijatimia katika nyakati zote. Hatujawahi kuwa nayo huko nyuma. Chunguzeni historia. Kamwe haijawahi kutokea. Nayo ilifanyika wapi, inapaswa kwenda wapi katika siku za mwisho? Kwa Kanisa teule. Si Babeli, si Sodoma; wao walikuwa na mjumbe kule chini. Lakini Roho Mtakatifu ndiye Mjumbe kwa Kanisa teule, usiku wa leo, Mungu akiishi katika mwili wa kibinadamu, akijionyesha Mwenyewe, Mtambuzi, Neno linalotambua mawazo na makusudi ya moyo. "Yesu Kristo yeye yule jana,

leo, na hata milele." Yeye ni Yehova-Yire. Yeye tayari ametupa Sadaka yetu, na anathibibitisha agano Lake. Yeye anatimiza agano Lake, katika siku za mwisho, kwa watu.

153 Wapendwa, tungeweza kuzungumza hapa usiku kucha. Mambo ambayo yamesemwa, yamesemwa ya kutosha. Wapo watu hapa walio wagonjwa; mnahitaji uponyaji. Kwa nini hamwamini jambo Hilo? Kama ningaliweza kuwaponya, ningalifanya jambo hilo. Iweni katika kuomba. Kama ningaliweza kuwaponya, ningalifanya hivyo. Mimi siwezi kuwaponya ninyi. Mimi ni . . . Mnaona, ninatoa huduma, usiku wa kwanza ama wa pili, hapa, katika kuwaombea wagonjwa. Na hilo si kwa ajili ya jambo hilo tu. Kama kuna Uzao wowote hapa uliokusudiwa Uzima, Roho Mtakatifu ataupata. Wataliona. Watalijua. Sasa Yeye ni . . .

154 Ni wangapi hapa mngeinua mikono yenu, mbele za Mungu, na kusema, "Ninaamini jambo hilo kwa moyo wangu wote, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele; ya kwamba amefufuka katika wafu, naye yu hai miongoni mwetu usiku wa leo, akijionyesha Mwenyewe kuwa yupo miongoni mwetu, nami ninaamini ni mambo ya Mungu"? Je! mngeweza kuinua mikono yenu, na kusema, "Kwa kweli ninaamini jambo hilo"?

155 Sasa, Baba wa Mbinguni, wako mikononi Mwako. Wao ni . . . Wanadai ya kwamba wao ni Uzao wa Ibrahimu. Wao—wao wanataka, wa—wanataka baraka za Mungu. Na sasa nimewaambia, katika njia hii rahisi, ndogo. Nilianza kwenye somo langu, wala sikulimaliza. Lakini, Baba, wa—wanaona hapa, katika kule kumthibitishia Ibrahimu, ya kwamba Wewe ulimthibitishia ile ahadi, ukampa uthibitisho. Sasa kama ninii—kama Roho wa Kristo hayumo ndani yetu, basi sisi si wa Kristo hata kidogo. Wala tabia ya Kristo haiwezi kubadilishwa.

156 Naye ametwambia vizuri kabisa, na anaahidi mambo haya kulingana na Biblia, mahali pengi. Hata Agano la Kale liliahidi jambo hilo, katika Malaki 4, jinsi ambayo ingekuwa katika siku za mwisho, "Angeigeuza mioyo ya watoto irudie Imani ya baba zao," kama baba wa Kipentekoste, lile Fundisho la awali la Biblia, lile Neno la asili, jinsi lingefanya. Na kungekuwako na ishara, na ishara hii ingethibitisha, ingethibitishwa na Sauti ambayo ingeifuata, ya kwamba Wewe upo hapa. Nasi tunakuamini.

157 Sasa, Baba, ja—jalia Shetani aondoke aende zake. Ha—hatuamini ya kwamba tuna nguvu zozote, Bwana. Hatudai kwamba tuna nguvu. Tunadai kuwa na mamlaka.

158 Tunatambua, yule polisi mdogo barabarani, akiwa amevaa kofia ndogo kichwani mwake. Na magari makubwa yakienda kasi kwenye barabara zilizo pana sana, maili tisini kwa saa, yakienda kwa mota yenye nguvu za farasi mia tatu, yeye hana

nguvu za kusimamisha moja ya hayo. Yangemkanyaga papo hapo chini kabisa kabisa. Walakini hebu na aonyeshe hiyo beji, na kuinua mikono yake, breki zitalia na tairi zitavuma. Ni mamlaka. Mji mzima uko nyuma yake. Yeye ana mamlaka, siyo nguvu. Huenda asiwe na uzito wa ratili mia moja, bali ana mamlaka.

159 Na hivyo ndivyo ilivyo usiku wa leo, Bwana. Tunamjia Shetani, si kwa nguvu, bali kwa mamlaka, tukionyesha Damu na thibitisho la lile agano. Yeye hana haki ya kuwashikilia watu hawa wagonjwa.

160 Nikiwaangalia na kuwaona wakitoa jasho, hapa, Ee Mungu, laiti kungalikuwa na njia fulani ninayoweza kuwaletea Ujumbe! Laiti wangaliweza tu kuona, Bwana, watambue tu! Waamshe, Bwana. Mara moja sasa, usiku wa leo, jalia waone ya kwamba Wewe ni Mungu yule yule. Unalithibitisha Neno Lako. Unalitimiza kama tu ulivyoahidi. Katika siku hizi za mwisho, ulisema mambo haya yangetukia, "Wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa," ya kwamba mambo haya yangetendeka. Tujalie, Bwana, na jalia waone ya kwamba ni Wewe. Katika Jina la Yesu, ninaomba. Amina.

161 Sasa aminini, enyi marafiki. Ninyi ni kusanyiko zuri sana. Ndio kwanza nipitilize wakati wangu, mnaona, wala si—sikumaanisha kufanya hivyo. Niliwaambia ni-. . . tutawahi kutoka, usiku wa leo, bali nilishindwa kwa sababu ni-. . . Nami nitamalizia somo langu kesho usiku, labda, Bwana akipenda.

162 Sasa tupo hapa. Ninyi ni watu. Sisi sote ni wanadamu tu. Tunataka kuishi. Kila mtu anataka kuishi amalizie muda wake. Ninaamini Mungu anataka tufanye hivyo. Ni—ninaamini jambo hilo. Sasa, si kwamba hapana Zeri katika Gileadi.

163 Unajua, ilisemwa wakati mmoja, "Kwa nini, ni kwa nini? Je!—je! hapana zeri katika Gileadi?"

164 "Huko hakuna nabii?" Isaya alisema, ama, ninamaanisha Eliya alisema. "Nenda kamwulize, 'Je! ni kwa sababu hakuna nabii katika Israeli? Kwa nini unapanda kwenda kule Ekroni, mungu Baal-zebubu? Kwa nini, mbona, unataka kwenda kule juu?' Yeye akiwa ni Myahudi, 'Kwa nini unapanda kwenda kule juu?'"

165 Kasema, "Je! ni kwa sababu hapana zeri katika Gileadi, huko hakuna tabibu kule? Yuko? Hiyo ndiyo sababu?"

166 Je! hiyo ndiyo sababu? La, Bwana. Tuna Zeri. Roho Mtakatifu yupo hapa. Naam, bwana. Ahadi ni yetu. Sasa inakubidi tu kuiamini. Ninyi . . .

167 Ni siku ambayo akili za watu zimetawanyika sana, hawaninii . . . Ninawasikitikia. Hawajui waamini kitu gani. Mmoja anasema *hivi*, na mwingine anasema *vile*. "Na kila neno la mwanadamu na liwe uongo, na Langu liwe kweli," Bwana

Mungu alisema. Hiyo ni kweli. Sasa Yeye hawezi kubadilisha tabia Yake.

168 Sasa, ninaamini jana usiku tulianzia na kadi ya maombi namba moja (sivyo?), na tukaita hadi ishirini, ama kitu kama hicho. Ati? Hebu tu na tubadilishe utaratibu huo. Hebu na tusiwe na kadi zozote za maombi. Naam, ombeni tu. Unajua, kadi ya maombi inakuleta tu hapa juu.

169 Lakini nahisi Uwepo Wake, kwa hiyo ninajua tu Yeye yupo hapa. Ni wangapi waliowahi kuona picha ya yule Malaika wa Bwana? Kwa hiyo nisaidie, nitakapokutana nanyi kwenye ile Hukumu, Yeye hayuko futi mbili kutoka mahali ninaposimama papa hapa. Hiyo ni kweli. Yupo hapa.

170 Sasa mtu asiye na kadi za maombi, inua mkono wako, useme, "Sina kadi za maombi, na hata hivyo mimi ni mgonjwa na mhitaji." Vema, ni kila mahali tu. Vema.

171 Sasa nitawaambia. Yule Malaika alifanya nini kule juu wakati ule? Aligeuza mgongo Wake, mgongo wake ulikuwa umegeuzwa kuelekea kwa Ibrahimu. Ambalo, nilitaka kulifikia, usiku wa leo, wala sikulifikia. Na pale aliposema, "Lingekuwa ni jambo lilo hilo atakapokuja Bwana, kama ilivyokuwa kule Sodoma." Tunaona, Yeye alikuwa amegeuza mgongo wake kuelekea kwenye hema. Na Sara akacheka yale aliyosema, kwa maana Yeye alimwambia. Wala asingeweza kufahamu ya kwamba huyo, akiwa tu ni Mwanadamu huko nje, akila nyama aliyokaanga, akinywa maziwa toka kwa ng'ombe, na akila nyama ya ndama wake, na huyo alikuwa ni Mungu.

172 Biblia ilisema alikuwa ndiye. Ibrahimu alisema alikuwa ndiye, "Elohimu." Hiyo ni kweli. "Elohimu," *Mungu*. Alitoweka moja kwa moja mbele ya Ibrahimu. Na, "Mungu," alimwita, "Bwana Mungu, Elohimu, Yeye ajitoshelezaye kwa yote."

173 "Hapo mwanzo," neno lile lile linatumika. Msomi yeyote anajua hilo. "Hapo mwanzo *Mungu*," angalia hicho Kiebrania, "Elohimu."

174 Angalia wakati Ibrahimu aliposema, "Bwana Mungu, Elohimu," Mtu yule yule, Mtu yule yule, akionyesha ya kwamba Mungu atajidhihirisha katika mwili wa kibinadamu, kwa Uzao wa Ibrahimu, kuthibitisha lile agano, na kufanya jambo lile lile alilofanya, (unaona hilo?) jambo lile lile alilofanya pale. Yeye daima ni nabii anayetambua mawazo na makusudi ya moyo. Kwa sababu, ni wangapi wanaojua Biblia ilisema ya kwamba, "Neno la Mungu linatambua mawazo yaliyo ndani ya moyo"? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

175 Sasa kama Mungu atachukua angalau watu watatu humu ndani, usiku wa leo. Sasa hii ni changamoto. Kama mtu yeyote hadhani hivyo ndivyo ilivyo, wewe njoo ulifanye jambo hili. Wasipokuja, basi msiseme neno kulihusu. Mnaona? Sasa, angalieni, tukichukua angalau watu watatu, (tatu ni thibitisho),

ambao siwafahamu kabisa, na kama Roho Mtakatifu. . . Kama utaamini tu, hilo tu ndilo ninalowaomba kuamini, kufanya, ni kuamini ya kwamba Biblia *hii* ni Kweli, nasi tunaishi katika siku za mwisho, na hii ndiyo ahadi ya siku za mwisho.

176 Kumbukeni, Ibrahimu, ama hakuna mtu mwingine, aliyeona ishara nyingine yoyote mpaka yule Mwana aliyeahidiwa alipojitokeza jukwaani. Ibrahimu aliona kila namna ya ishara na kadhalika, kufikia wakati huo, bali hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho. Yeye kamwe hataukatiza; ule mwendeleo wa Mungu. Uzao wa Ibrahimu, hiyo ndiyo ishara yao ya mwisho. Unaona? Hiyo ilikuwa ndiyo ya mwisho. Mungu! Yeye alijua, papo hapo, huyo alikuwa ni Elohimu. Naye Yesu akarudi moja kwa moja na kusema ingekuwa hivyo, na sisi tupo papa hapa leo kwenye hilo, jambo lile lile.

177 Enyi watu, hii ni Kweli. Ninajua, "Papa hapa katika shedi ndogo?" ulisema. Vema, imekuwa hivyo daima. Yeye alizaliwa katika hori. Ilikuwa ni vigumu kupata mtu yeyote angalimwamini. Lakini ni Uzao ule tu unaoamini, ambao umekusudiwa Uzima, hao peke yao. "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Hiyo ni kweli. Huna haja ya kuwa na wasiwasi, kwamba; jina lao liko, wataliona. Na kwa jinsi gani? Wataliona.

178 Sasa, mnaona, ni wazo tu, ni—ningeweza kuomba na kuwawekea mikono. Nitazungumzia jambo hilo, hasa Jumapili alasiri. Lakini ni—ninawataka mwone ya kwamba mnaweza kuweka mikono yenu juu Yake. "Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana na mambo ya udhaifu wetu." Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaamini. Na sasa kama Yeye atafanya jambo hilo . . .

179 Ni—ninamjua mtu fulani hapa. Imetokea tu niliangalia huko, nami ninaona wawili ama watatu wa rafiki zangu wameketi moja kwa moja pale, ambao ni mhudumu, baadhi yao pale. Na mmoja aliyeinamisha kichwa chake, ndio kwanza Bwana amponye mvulana wake mdogo, kutokana na jeraha la bongo, bado, leo, alinipigia simu.

180 Na—na mtu mwingine pale, na maskini mtoto wake mchanga, hivi juzi usiku, walidhani alikuwa amekufa. Nami nilikuwa huko Beaumont. Na sisi, tukapiga simu, tukaenda kule, na akaweka mikono yake juu yangu, akaanza kulia, kasema, "Ndugu Branham, Neno la Bwana liko pamoja na wewe. Mwombe tu." Na dakika hiyo hiyo, mtoto huyo mchanga akafufuka, na akaanza kuishi tena. Yule pale baba yake ameketi pale moja kwa moja, mhudumu.

181 Na mtu huyu, gari lilipata ajali ya barabarani, naye akatupwa kupitia kitu fulani ama kingine, na kurushwa kwenye handaki, ndipo likajeruhi maskini ubongo wake, na kadhalika.

Bwana alimponya, mzima kabisa. Waliamini. Kweli kabisa wao. . .

182 Sasa msiseme ya kwamba mimi nilifanya jambo hilo. Sikuwa na uhusiano wowote nalo. Imani yao katika Mungu, hiyo ndiyo ilisababisha jambo hilo. Iweni na imani! Nyote. . .

183 Yesu alisema, katika Marko 11:22, "Jambo lolote! Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usione shaka moyoni mwako, ila uamini kwamba hayo uliyosema yatatukia, yatakuwa yako." Hata hivyo hilo hapo, unaona. Siyo tumaini; ni suala la "kulijua hilo."

184 Na kama Yeye anaweza kujithibitisha kwamba Yu hai, Yule aliyefanya hiyo ahadi anaweza kuthibitisha kwamba Yeye yu hai, wala hakuna kitu kingine ulimwenguni kinachoweza kufanya jambo hilo. Amkeni! Jitikiseni, kwa nguvu sana, roho yenu. Mnaona? Hakuna kitu ulimwenguni kinachoweza kufanya jambo hilo ila Mungu.

185 Sasa unaweza—unaweza kujiamulia kwamba ni yule mwovu, ukitaka. Watu walimhukumu Yeye kwamba ni mwovu, kwa hiyo wangali wanaweza kumhesabu Roho Wake kwamba ni mwovu. Wao walisema, "Yeye alikuwa ibilisi, aliyekuwa akitenda hayo." Vema, hakuna budi, walipata thawabu hiyo.

186 Ninyi aminini tu. Hamwezi kuponya. Siwezi kuponya. Hakuna mtu anayeweza kuponya. Mungu ndiye mponya.

187 Bali kama tu unaweza kutambua ya kwamba Yeye yule unayemtumikia, na ambaye umejitenga na ulimwengu upate kumtumikia, yeye yule unayempenda; yeye yule hasa atakayesimama kwenye ile Hukumu, wewe ukiwa Hukumuni pamoja Naye, upate kuhukumiwa, kama Uwepo Wake unaweza kuja papa hapa na kuonyesha ya kwamba Yeye yupo hapa!

188 Sasa mwili Wake wa kibinadamu hauwezi kufanya hilo. Wakati huo utakapokuja, wakati umekwisha. "Kama vile umeme utokavyo Mashariki hadi Magharibi, ndivyo itakavyokuwa kuja Kwake Mwana wa Adamu." Isipokuwa, Roho Wake tu!

189 Na Kanisa limekuja, angalia vile limekuja; kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu; na sasa moja kwa moja kufikia wakati wa kunyakuliwa, kuliweka Kanisa tayari. Vile hasa lilivyoahidi, jinsi hasa ambavyo Nyakati za Kanisa zilivyopangwa, nasi tumeona jambo hilo, kila kitu kikishuka kuja moja kwa moja, na moja kwa moja.

190 Pentekoste ndilo dhehebu la mwisho. Hilo ni kulingana na Maandiko. Litakuwa ndilo dhehebu la mwisho, limekataliwa pamoja na hayo mengine, hiyo ni kweli, kama dhehebu. Hakuna dhehebu linalokubalika kwa Mungu. Ni ninii. . . Ni watu binafsi, ndio wanaokubalika kwa Mungu.

191 Sasa je! hamwezi kuamini Uwepo Wake? Sasa hapa, mimi ni ndugu yenu tu, na sasa nilitumwa, ambapo Mungu aliniambia nije nifanye jambo hili. Kwa hiyo, ninamwamini. Na kama halikuandikwa katika Neno, kwa ajili ya wakati huu, ningeliliacha. Chochote ambacho hakiko kwenye hilo Neno, sikiamini. Ni—nisingelikikubali. Sisemi nisingelikiamini, bali sikikubali; sikielewi. Lakini wakati kiko kwenye Neno hili, na ni ahadi kwa ajili ya wakati huu, ninakifahamu. Nanyi je? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Bwana na atusaidie sasa. Nanyi mninii tu . . . Ninyi karibieni sasa, kwa imani, aminini kuwa katika ninii . . . uwepo wetu . . . Tuko katika Uwepo Wake, hasa, sasa, ni Yesu yule yule aliyefanya ahadi hiyo.

192 Na katika Biblia hapa, yule Paulo aliyevuviwa, ambaye alikuwa amepata funuo kwa wingi sana hata alishikwa na wasiwasi, "Naye alikuwa na shida katika mwili wake, asije akajivuna kwa wingi wa hizo funuo." Unaona, yeye aliandika Biblia, alikuwa amevuviwa sana. Aliandika vitabu vya Biblia. Kama vile Musa, yeye alikuwa ni nabii. Kwa hiyo yeye, Neno lilimjia, naye akaliandika, na likakubalika katika Maandiko, Maandiko matakatifu. Sasa yeye ndiye ambaye—ambaye—ambaye anasema ninii . . . anaamini jambo hili, aliyefundisha mambo haya.

193 Sasa kumbuka ya kwamba Kristo amefufuka katika wafu na yuko miongoni mwetu. Basi shika hilo moyoni mwako, Kristo alifufuka katika wafu na yuko miongoni mwetu.

194 Sasa, tumeona kila namna ya miamsho mikubwa, na kupaaza sauti na kumsifu Mungu; yote ni sawa. Tumenena kwa lugha na kutabiri, na kadhalika. Tumeona hayo yote. Hayo ni sawa. Hayo yanaambatana moja kwa moja na jambo Hilo.

195 Lakini, kumbuka, jambo la mwisho ni Uwepo Wake wa Kiungu, Neno Lenyewe. Yeye ni Neno. Kichwa, Neno, kinakuja kwenye Mwili. Mnaona? Halafu basi Neno hilo, katika Waebrania mlango wa 4, lilisema, "Neno la Mungu ni kali, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, na huyatambua mawazo na makusudi ya moyo." Sasa hebu chukua Andiko hilo na ulifuatilie huko nyuma kutoka mwanzo wa manabii, ulifuatilie moja kwa moja kupitia kwa Yesu Kristo, uone kama si jambo lile lile, jambo lile lile, kwamba Yeye anajulikana kama Masihi.

196 Sasa si kwamba mtu fulani hapa ndiye Masihi. Roho Mtakatifu ndiye Masihi. Kristo na Roho Mtakatifu ni kitu kile kile, kwa hiyo huyu papa hapa sasa akifanya kazi katika mwili, akiutayarisha huo Mwili kwa ajili ya neema ya kunyakuliwa. Liaminini, wapendwa.

Bwana Mungu, tafadhali jalia litukie usiku wa leo.

197 Sasa katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Ninasema hivyo ili mpate kufahamu. Mnaona, msininii . . .

198 Kama unatilia shaka, wewe—wewe, si vyema kukaa sana, maana watu wengi walioketi hapa, hapana shaka, wameona ni jambo gani linalotukia mara nyingine kwa wasioamini. Atatoka kwa mtu mmoja aingie kwa mwingine, kama ilivyotukia katika Biblia.

199 Ni wangapi wenu hapa wanaoomba, wanajua ya kwamba siwafahamu, mimi sijui lolote kuwahusu? Inueni mikono yenu, ya kwamba mnaomba, basi unajua kuwa sijui lolote kukuhusu wewe.

200 Wewe, mtu yule anayeketi pale amevaa tai nyeusi, akiniangalia moja kwa moja hapa.

201 Sasa angalieni. Mnaiona ile Nuru? Hamwezi kuiona Ile? Ni Nuru tu ya rangi ya kaharabu, yenye rangi ya dhahabu na ya kijani kibichi hapa chini.

202 Je! unaniamini mimi kwamba ni mtumishi Wake, bwana? Kama Mungu anaweza kunifunulia kwamba una shida gani, je! unaamini, ungeniamini mimi kwa moyo wako wote, ungeamini ilikuwa ni Mungu? Ungefanya jambo hilo? Ungeamini uponyaji wako ungekuja? Je! una kadi ya maombi? La, huna. Huihitaji. Shida yako iko kwenye sikio lako. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Ilikuwa kwenye sikio lako, haiko sasa, kama ukiamini. Simjui mtu huyo, sijawahi kumwona.

203 Sasa huyu hapa mtu anayeketi papo hapo karibu na wewe. Kwa namna fulani anaomba. Anaombea shida fulani aliyo nayo. Niangalie, bwana. Je! una kadi ya maombi? [Ndugu huyo anasema, "La."—Mh.] Huna. Je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? ["Ndiyo."] Je! unaamini yale nimekwambia, ni Kweli? ["Ndiyo, bwana."] Unaamini ni Uwepo wa Yesu Kristo? ["Ndiyo, bwana."] Je! unaamini mgongo wako utapona tangu sasa na kuendelea? Unaamini? Inua mkono wako. Kama utaamini! Unaona?

204 Sasa mwulizeni mtu huyo. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Yeye kamwe hakunigusa. Yuko futi ishirini kutoka kwangu. Je! aligusa nini? Hilo linatimiza Maandiko. Yeye alimgusa Kuhani Mkuu. Alikuwa ameketi pale, akiomba apate kuponywa. Unaona, alimgusa Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu. Mnaona?

205 Sasa, unafikiri nini, ewe kijana mwanamume unayeketi huko nyuma, kijana anayenikazia macho moja kwa moja? Je! unaamini Mungu aliponya ugonjwa huo wa figo ulio nao? Unaamini? Inua mkono wako, kama unaamini jambo hilo. Je! unataka kukomesha tabia hiyo uliyo nayo, pia, uzitupilie mbali sigara hizo? Tikisa mkono wako namna *hii* kama unataka. Kisha uweke chini na uzisahau. Yesu Kristo alikuponya. Kama unaweza kuamini!

206 Papo hapo upande wako wa pili, yupo mama anayeketi aliyevaa miwani. Anaugua ugonjwa wa wasiwasi. Je! unaamini

Mungu atakuponya, mama? Inua mkono wako kama unaamini. Vema.

207 Tafadhali? Yupo kijana mwanamke anayeketi papo hapo karibu na wewe, ana ugonjwa wa kike, ugonjwa wa akina mama. Hiyo ni kweli, mama. Inua mkono wako, kama hiyo ni kweli. Mtiririko. Weka mkono wako juu yake, apate kupona, maana anaamini.

208 Hebu, halafu anayeketi karibu naye, moja, mbili, Hiyo hapo moja kwa moja juu ya mama huyo mwingine anayeketi papo hapo karibu naye. Anaumwa na miguu yake, ugonjwa wa miguu yake. Je! unaamini Mungu ataiponya miguu yako? Inua mkono wako. Haya basi. Unaona?

209 Mnamwamini Yeye kwamba ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

210 Je! unaamini, unayeketi pale? Papo hapo nyuma ya mtu huyu anayeketi hapa mbele, mama anayeketi *hapa*? Je! unaamini ya kwamba Mungu . . . Una vitu viwili vya hatari. Kimoja cha hivyo ni kansa; hicho kingine, ni yabisi kavu. Je! unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Kama utaamini, inua mkono wako na useme, "Ni—Ninaamini." Vema, amini.

Je! mnaamini? Yeye anathibitisha lile agano.

211 Huyu hapa mama mmoja anayeketi hapa akiniangalia, papa hapa nyuma ya mtu huyu. Amevaa nguo inayoonekana nyekundu kidogo. Nyekundu, *hapa* juu, fulana, huenda ikawa ni fulana. Yuko mbali sana; mwanga umepungua kule. Baada, unaona, hilo linakufanya dhaifu sana, kitu hicho chote kinaanza kugeuka kuwa namna fulani ya rangi ya maziwa kote humu chumbani.

212 Ambayo, Hiyo pale imesimama, moja kwa moja juu yake. Mnaiona ile Nuru? Yeye anaombea jambo fulani. Kama Yesu Kristo atanifunulia kile unachoomba, je! utaamini kwa moyo wako wote? Utaamini? Sikufahamu, nawe hunifahamu. Lakini umewasiliana na Kuhani Mkuu, maana ishara anayonipa mimi iko moja kwa moja juu yako, unaona, unaona, ile ishara. Ninajua ndivyo ilivyo.

213 Unaugua ugonjwa mbaya sana wa wasiwasi. Na pia una tezi kooni mwako, inayokuuma. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

Unasema, "Unaweza kuiona hiyo."

214 Vema, unatoka . . . Wewe hutoki hapa. Unatoka . . . Hutoki katika nchi hii hapa, mahali hapa. Umetoka Memphis. Hiyo ni kweli.

215 Huyo mama anayeketi karibu na wewe, yeye pia ametoka Memphis. Je! unaamini kwa moyo wako wote, mama? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya? Je! unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama mtumishi Wake? Hilo huwakwaza watu, unaona. Je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Je!

unaamini ya kwamba Mungu ndiye anayesema maneno haya? Unajua mimi nisingejua lolote kukuhusu wewe. Je! unaamini ingekuwa ni Mungu basi? Vema. Amini kwa moyo wako wote. Na una ninii, kinachokusumbua, una ninii . . . una shida ya koo lako, pia. Na jambo lingine, una kifundo, uvimbe ubavuni mwako. Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia uko upande gani? Kama ndivyo ilivyo, inua mkono wako kama nitakwambia ukweli. Uko upande wa kulia. Unaona? Unaona? Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Je! hilo litakusaidia? Wewe ni Mke wa Cox. Hiyo ni kweli. Unaona? Rudi, unaona.

216 Je! mnaamini? Nyote mnaamini sasa? [Kusanyiko linafurahi na kusema, "Amina."—Mh.] Mnaona, hilo ni thibitisho la agano kwa Uzao wa Ibrahimu, kama mnaweza kuamini! Mnaona?

217 Hapa, yupo maskini mwanamke anayelala hapa kwenye machela. Je! unaweza kunisikia, mama, unayelala kwenye machela hiyo? Naam. Siwezi kukuponya. Sijui lolote juu yako; wewe ni mgeni tu kwangu. Lakini je! unaamini ya kwamba Yesu Kristo anaweza kunifunulia kwamba shida yako ni nini? Hilo lingekusaidia? Lingekusaidia, sivyo? Kama ukilala hapo, utakufa. Una nafasi moja tu ya kuishi, hiyo ni kumkubali Kristo. Una kansa. Hiyo ni kweli. Je! unaamini ya kwamba Mungu atakuponya sasa? Unaamini? Inua mkono wako kama unaamini. Vema. Mahali hapo ulipo, jambo pekee ambalo ungaliweza kufanya, lingekuwa ni kusimama na kutoka kwenye kitanda hicho; na kuchukua kile unacholalia, na uende nyumbani, ukidai imani yako katika Mungu, kama Mzao wa Ibrahimu. Simama, katika Jina la Yesu.

Unaona, anasimama, apate kuchukua ahadi yake katika Mungu.

218 Ni wangapi wenu ninyi wengine mnaoamini kwa moyo wenu wote sasa?

219 Simama. Una nguvu; Mungu atakupa nguvu. Simama, kwa miguu yako. Huyo hapo, amesimama, ametoka kwenye machela.

220 Sasa ninyi wengine mnaotaka kumpokea Yesu Kristo, simameni kwa miguu yenu. Simameni kwa miguu yenu. Simameni, kila mahali, mkubalini Yesu Kristo kama mponya wenu.

221 Bwana Yesu, mponye kila mmoja wao. Tujalie, Bwana.

*YEHOVA-YIRE 1* SWA64-0402

(Jehovah-Jireh 1)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 2 Aprili, 1964, kwenye Kibanda cha Klabu 4-H huko Louisville, Mississippi, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2013 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org